# Nipashe

Ijumaa Septemba 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581420

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



tigo pesa SportPesa

MAOKOTO Deilee!

WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Bodaboda** kutunukiwa kwa kunusuru majeruhi ajali gari la wagonjwa akilifikisha hospitalini

UKURASA 3


BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Waziri Ulega: linakuja na neema kwa wafugaji, wavuvi, wazalishaji nyama

KONGAMANO KIMATAIFA LA CHAKULA AFRIKA

Dk. Samia alivyoanza safari mapema, kilimo nchini chasonga bajeti 330%

UKURASA 11

JUKWAA LA KATIBA:

# Mchakato wa Katiba Mpya usisubirishwe

UKURASA 2



Bob Wangwe Pindi Chana Ananilea Nkya

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

## ‘Mke wa Bilionea Msuya alikuwa na ugomvi wa mali na wifi yake’

UKURASA 4

# Rais Samia: Tuwalinde watoto wetu, taifa litakosa uendelevu

UK. 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza jambo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa Kilele cha Tamasha la Kizimkazi, Paje Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

MICHEZO YANGA YAFICHUA SIRI YA KUGAWA ‘5G’ UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# JUKATA yataka mchakato Katiba mpya usisubirishwe

**Na Enock Charles**

SERIKALI imeshauriwa kuacha mpango wa kutoa elimu kuhusu Katiba badala yake kutoa ratiba ya mchakato wa katiba mpya ili kuondoa sintofahamu iliyopo kwa wadau kuhusu hatima ya jambo hilo.

Pia imeshauriwa kufanya marekebisho madogo katika sheria za uchaguzi ili kufanyika uchaguzi huru na haki wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ifikapo mwakani na mwaka 2025.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam kwa Waziri mpya wa Wizara ya Katiba na Sheria, Balozi Pindi Chana, kutokupoteza muda na fedha za umma katika suala la elimu kwa kile alichosema elimu ilishatolewa tangu mwaka 2011.

"Suala la elimu ya Katiba kwa wananchi lilikwishafanywa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba.

Kwa hiyo kinachotakiwa kwa sasa ni ratiba ya hatua za mchakato," alisema Wangwe.

Mkurugenzi huyo alitoa sheria za mfano za kuongoza mchakato wa katiba zilizoandaliwa na jukwaa hilo ambazo ni sheria ya marekebisho ya katiba na sheria mfano ya kura ya maoni pamoja na nyaraka zinazotoa ufafanuzi juu ya sifa za upatikanaji wa kamati ya wataalamu na namna bora ya usimamizi na utatuzi wa migogoro inayoweza kutokea katika hatua za mchakato wa Katiba Mpya.

"Sheria hii mfano ya mchakato wa Katiba imetoa hatua za mchakato, upatikanaji wa kamati ya wataalmu na majukumu yake. Pia imeainisha namna migogoro inavyoweza kutatuliwa na kusimamiwa katikati ya mchakato na imependekeza masuala ya kibajeti na vitu gani vinaweza kufanyika katika hatua za mpito wa nchi kupata Katiba Mpya," alisema.

Mwenyekiti wa JUKATA, Dk. Ananilea Nkya, alipendekeza kufanyiwa marekebisho sheria zinazosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ili uwe huru na wa haki hata kama Katiba Mpya itakuwa bado haijapatikana kufikia mwakani na mwaka 2025 ili kupata viongozi bora.

"Hata kwa mfano mchakato ukaanza mwezi huu inaweza ikafika mwakani ikawa katiba haijakamilika na kuwepo sheria za kuendesha uchaguzi kupitia katiba mpya. Yafanyike marekebisho madogo kwenye Katiba ya sasa ili uchaguzi unaokuja mwakani wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ufanyike kwa uhuru na haki," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema viongozi bora walioopatikana kwa uchaguzi huru na haki ni rasilimali namba moja katika maendeleo ya nchi, hivyo kutaka kuharakishwa kwa maboresho ya sheria za uchaguzi ili kuongoza uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Katika taarifa yake kwa waandishi wa habari Jumatatu iliyopita, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema wizara imekuja na mpango wa kutoa elimu kwa wananchi kwa miaka mitatu ili wananchi waielewe vyema Katiba ya mwaka 1977.

Alisema hatua hiyo itasaidia wananchi kutoa michango chanya katika mchakato huo, jambo ambalo limepingwa vikali na wadau mbalimbali.




Mufti wa Tanzania, Abubakar Bin Zuber (kushoto), akizungumza wakati wa mkutano na taasisi za Kiislam kujadili somo la elimu ya dini , kufundishwa katika shule za Umma nchini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Samia: Tuwalinde watoto, Taifa litakosa uendelevu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesisitiza umuhimu wa kulinda watoto kimaadili kwa maslahi ya taifa, akionya kuwa wasipolindwa Taifa litakosa uendelevu.

Aliagiza hayo jana alipofunga Tamasha la Saba la Kizimkazi lililofanyika Paje, Mkoa wa Kusini Unguja, viongozi mbalimbali wa kiserikali zote mbili wakihudhuria pamoja na viongozi wa dini, kisiasa na wananchi.

Rais alisema ili kudumisha utamaduni, mila na desturi, ni lazima kuhakikisha tamaduni na mila hizo zinarithishwa kwa watoto.

Alisema ni lazima watoto wafundishwe na kukuzwa katika maadili mema ili kuwa na Taifa lenye nidhamu na uwajibikaji kwa sababu msingi wa Taifa lolote unaaza kwa watoto.

"Katika kufanya hivyo, katika tamasha hili tumezingatia mambo kadhaa ambayo tunaona ni vyema yakarithishwa kwa watoto wetu, ikiwamo lugha ya Kiswahili, vyakula vya asili kwa sababu baadhi ya vyakula hivyo vimeanza kutoweka," alisema.

Mkuu wa Nchi alitolea mfano vyakula vya asili vilivyoanza kutoweka ni makopa ambacho ni maafuru katika Wilaya ya Kusini Unguja.

"Baadhi ya vyakula vimeanza kutoweka, leo ukipika chakula cha makopa wajukuu hawajui, utasikia wanasema bibi leo umepika muhogo mbovu, kumbe ni chakula mahsusi kwa huku kwetu Kusini (Unguja)," alisema.

Rais pia alisema lazima watoto warithishwe kazi za kiuchumi, katika tamasha hilo kulioneshwa kazi kadhaa za kiuchumi zinazofanywa katika Mkoa wa Kusini ili watoto warithi shughuli hizo.

Pia alisema kuna tamaduni za ngoma na nyinginezo ambazo watoto hawana budi warithishwe, ikiwamo ngoma za asili na resi za ngalawa.

Alisema katika tamasha hilo la mwaka huu miradi mbalimbali imezinduliwa na mingine kuwekewa mawe ya msingi ikiwamo ya sekta za elimu, afya na utalii, akiwashukuru wadau na washirika wote wa maendeleo katika kuimarisha sekta hizo za maendeleo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema tamasha hilo limeanza kuonesha sura ya kuimarisha maendeleo na kutoka nje ya Tanzania, hivyo ni muhimu kwa serikali zote mbili kuliweka katika ratiba ili kuongeza idadi ya watalii.

Alisema kwa kufanya hivyo litaleta mzunguko wa kifedha katika maeneo hayo. Alimpongeza Rais kwa kazi nzuri ya kulitumikia Taifa.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Masoud Othman Masoud, alisema uongozi si nguzo wala silaha, bali ni heshima na upendo wa watu. Wananchi wana imani na Rais Samia jinsi inavyoendesha nchi.

Alisema Mkoa wa Kusini Unguja ndiyo mkubwa kwa Zanzibar na una sifa nyingi ikiwamo vivutio vingi vya utalii na Hifadhi ya Msitu wa Jozani ambao mbali na hifadhi, lakini kimataifa umepewa hadhi wa kuwa msitu wa bayonuai.

Othman alisema tamasha hilo limawaonesha njia Wazanzibari kuzitumia rasilimali zilizopo na kuondokana na njaa kwa sababu milango ya uwekezaji na uchumi imefunguka.

Akiwasilisha salamu za Baraza la Vyama vya Siasa katika tamasha hilo, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abrahman Kinana, alisema vyama vya siasa vinampongeza Rais Samia kwa namna anavyoongoza nchi, alivyoleta maridhiano na kuimarisha umoja wa taifa.

**UZINDUZI TAWI NMB**

Katika hatua nyingine, Rais Samia amezindua tawi la Benki ya NMB Paje, Mkoa wa Kusini Unguja, uzinduzi unaoendelea kupanua mtandao wa matawi ya benki hiyo nchini na kufikia 230 yanayotumika kutoa huduma kwa zaidi ya wateja milioni sita.

Uzinduzi huo ambao ni sehemu ya tamasha hilo, umefanyika ikiwa ni siku 58 tangu Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alipozindua tawi la 229 la Benki ya NMB Buhigwe, mkoani Kigoma.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi waandamizi wa serikali ambao ukiondoa Rais Samia, pia walikuwapo Waziri Mkuu Majaliwa, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Viongozi wengine ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Moses Kusiluka, Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda pamoja na mawaziri mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

"Karibu kutuzindulia Tawi la NMB Paje, ambalo ni la nne hapa visiwazi Zanzibar, lakini likiwa ni la 230 kwa mtandao mzima wa matawi yetu nchini.

"Tuna imani kwamba tawi hili linakwenda kuwasaidia sana wakazi wa mahali hapa, ambao awali walikuwa wanasafiri umbali mrefu wa takribani kilomita 60 kwenda Mwanakwerekwe kufuata huduma zetu za kibenki katika tawi letu kule," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna alipomkaribisha Rais.

Baada ya maelezo hayo, Rais Samia alikata utepe kuashiria ufunguzi wa tawi hilo kabla ya kuingia ndani kukagua miundombinu na mifumo ya utoaji huduma ndani ya jengo hilo.

Akiwa ndani ya tawi, Rais Samia alitembezwa katika ofisi za vitengo na idara mbalimbali kisha kuingia katika Viwanja vya Paje alikozungumza na wananchi.

Tawi la NMB Paje linakuwa la tatu kufunguliwa na benki hiyo mwaka huu, likitanguliwa na matawi ya Kwa Mrombo, jijini Arusha (Mei 3) na Buhigwe, mkoani Kigoma (Julai 4).

HABARI KITAIFA



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akikabidhi tuzo kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kama mdau wa elimu, katika hafla ya kutambua mchango wa wadau katika sekta ya elimu, iliyoandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda. **PICHA: EMMALOVENESS GASTON/TUDARCo**

# Bodaboda amwokoa mjamzito kwa kuendesha 'Ambulance'

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linakusudia kumpa cheti cha kumpongeza mwendesha bodaboda, Seif Radhid (24) mkazi wa Bombambili, Manispaa ya Songea kwa kuokoa maisha ya mjamzito na mtoto baada ya gari la wagonjwa kupata ajali.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chiya, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 25, mwaka huu majira ya saa tatu asubuhi katika makutano ya barabara ya kutoka Matarawe kwenda Bombambili (Matarawe Junction).

Alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili T 626 BXU Toyota Land Cruizer, lililokuwa likiendeshwa na Lomwadi Peter (36) maarufu kwa jina la Kipaule, mkazi wa Kijiji cha Hanga wilayani Namtumbo.

Akielezea tukio hilo, Kamanda Chiya alisema kijana huyo alijaribu kuokoa maisha ya watu wawili, Edson Chalamila (21) mkazi wa Mkuzo, Manispaa ya Songea ambaye ni mwendesha bodaboda aliyegongana na gari la kubeba wagonjwa lililokuwa linamkimbiza mjamzito kwenda katika Hospitali ya Misheni Peramiho.

Alisema dereva Kipaule akitokea Hanga kuelekea Hospitali Peramiho, aligongana na mwendesha pikipiki ambayo ilitoroshwa baada ya tukio na ilikuwa ikiendeshwa na Chalamila ambaye alijeruhiwa na baadaye kufariki dunia.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa mwendesha bodaboda kutochukua tahadhari kwa watumiaji wengine wa barabara na dereva wa bodaboda alishindwa kutoa kipaumbele kwa gari ya kubebea wagonjwa ambayo ilikuwa imembeba mjamzito na baada ya ajali hiyo kutokea aliumia alishindwa kuendesha gari hiyo.

Alisema baadaye alijitokeza Seif aliyekuwa eneo la tukio aliangalia ndani ya gari na kuona dereva ametoka huku gari ikiendelea kunguruma na ufunguo ukining'inia ndipo alipoendesha gari hiyo kwenda hospitali umbali wa kilomita 25 kutoka Songea mjini.

Alisema aliwafikisha majeruhi na mjamzito, lakini baadaye Chalamila alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu.

"Alichokifanya kijana Seif ni cha ujasiri mkubwa kwani aliokoa maisha ya mjamzito na mtoto. Natoa wito kwa madereva wote wanaoendesha vyombo vya moto hasa magari ya kubebea wagonjwa pamoja na watembea kwa miguu kuchukua tahadhari wakati wawapo barabarani ili kuepuka madhara yatokanayo na ajali.

Wakati huo huo, watu 11 wa familia ya Mahona Kadoto ambao ni jamii ya wafugaji katika Kijiji cha Mtwana wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wamelazwa Katika Hospitali ya Tunduru na mtoto wa miaka mitatu, Rashidi Mahona akifariki dunia.

Alisema tukio hilo lilitokea Agosti 27, mwaka huu majira ya saa nane mchana katika kitongoji cha Majengo Kijiji cha Mtwana, Kata ya Luumbule.

Kamanda Chilya alifafanua kuwa inadaiwa siku hiyo ya tukio familia ya Mahona Kadoto yenye jumla ya watu 25 kati yao 11 walikula chakula kinachodhaniwa kuwa na sumu ambacho ni ugali na mchicha na ghafla walianza kuumwa tumbo baadaye walikimbizwa hospitalini.

Alisema baadhi ya wanafamilia wanaendelea na matibabu huku polisi wakiendelea na uchunguzi.

# Wasanii wamiminika kurudisha nguo za jeshi

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Wananchi Tanzania (JWTZ) limesema watu wengi wamejitokeza kurejesha sare za jeshi ikiwamo wasanii na waandishi wa habari.

Akizunguma na Nipashe jana, Msemaji Mkuu wa JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Ilonda, alisema kabla ya muda kukamilika wamejitokeza kwa wingi kurejesha sare hizo.

"Wengi wamejitokeza wakiongozwa na wasanii na waandishi wa habari walijitokeza jana kwa wingi (juzi) nilikuja kuzipokea na hata jana wamejitokeza kazi kubwa imefanyika ya kuzikusanya," alisema Ilonda.

"Watu wanatoa ushirikiano ukimkuta mtu ana begi wanatupatia wanaoenda kufuatilia hizi nguo wanakuwa wamevaa sare zetu na vitambulisho, wasiende watu ambao hawafahamiki ili wasiwasumbue wananchi hatutaki watu wasumbuliwe wanatoa nguo tunaondoka nazo kama ni begi wanakabidhi tunaondoka nazo," alisema Ilonda.

Aidha, alisema wataendelea kuzikusanya nguo hizo kadri ya watu wanavyojitokeza kutokana na wengine kusafiri nje ya nchi, kulazwa kwa matibabu ama kusafiri kikazi, kwa sababu hawawezi kusema wamekaidi agizo hilo. "Tutaendelea kupokea lakini wale ambao wataendelea kuzitumia tutawakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola," alisema Ilonda.

Agosti 24, mwaka huu, JWTZ ilitoa siku saba kwa wananchi kusalimisha sare za jeshi hilo kwenye vituo vya polisi au JWTZ.

Jeshi hilo lilisema kuwa wasanii ambao watahitaji kutumia mavazi hayo watatakiwa kuomba kibali ili waruhusiwe kuyatumia na baada ya siku saba atakayekutwa na mavazi hayo atachukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine.

# Mfanyabiashara madini, mwanawe wauawa kikatili

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MFANYABIASHARA wa madini, Marwa Masese anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 55 hadi 60 na mwanawe John Marwa (30), wakazi wa Kunduchi Mtongani, Dar es Salaam, wameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kwenye vichwa vyao.

Mauaji hayo yanadaiwa kuhusishwa na uhusiano wa karibu wa kibiashara.

Habari zilizopatikana jana mjini hapa na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, zinasema tukio hilo lilitokea Agosti 29, mwaka huu, majira ya saa 11:00 alfajiri katika kitongoji cha Mkerema, kijiji cha Lilondo, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Kamanda Chilya alisema inadaiwa siku hiyo ya tukio katika barabara kuu ya kutoka Njombe kwenda Songea yalitokea mauaji ya watu wawili waliouawa kwa kupigwa kwenye vichwa vyao. Alisema katika mauaji hayo, John Marwa alipigwa hadi kufumuliwa ubongo kwa kutumia kitu chenye ncha kali.

Alisema baada ya mauaji hayo kufanyika, watu waliotekeleza tendo hilo walichukua miili ya marehemu hao na kuiweka ndani ya gari lenye namba za usajili T 241 DSX aina ya Jeep Grand Cherokee lenye rangi nyekundu, mali ya Marwa Masese kisha kulisukumiza kwenye korongo ili ionekane watu hao wamefariki dunia kwa ajali ya gari.

Kamanda Chilya alisema Marwa alikuwa ametoka Dar es Salaam siku za nyuma na alikwenda hadi kwenye eneo la machimbo ya madini yaliyoko kijiji cha Amani Makolo, Mbinga mkoani Ruvuma ambako aliongozana na mtoto wake, John.

Alisema walipofika kwenye machimbo hayo ambayo Marwa ana zaidi ya vitalu 10, alikwenda kufanya mazungumzo na mwekezaji ambaye walikubaliana kuwa mwekezaji atakuwa anamlipa asilimia 30 ya madini anayoyapata kwenye vitalu hivyo.

Baada ya kukamilisha mazungumzo hayo, alisema Marwa na wenzake watatu, akiwamo mtoto wake, walianza safari ya kwenda Mbeya ambako pia kulikuwa na mazungumzo ya biashara ya madini.

Alisema baadaye, Marwa na wenzake walianza safari ya kutoka Mbeya kurudi wakiwa katika magari mawili tofauti kati ya Marwa na mtoto wake. Marwa alikuwa katika Jeep na mwanawe Toyota IST (namba za usajili zimehifadhiwa) akiwa na dereva ambaye anadaiwa ni mtu wa karibu wa Marwa na abiria wake ambao majina yamehifadhiwa kwa uchunguzi zaidi.

Kamanda Chilya alisema walipofika Njombe kwenye maeneo ya makutano ya barabara walisimamishwa na askari wa usalama barabarani kwa madai kukiuka sheria za usalama barabarani na kuandikiwa faini kisha wakaendelea na safari.

Walipofika katika kitongoji cha Mkerema, dereva aliyekuwa nyuma yao alionyesha ishara kuwa wasimame na baada ya kufanya hivyo, Marwa na mwanawe walianza kupigwa na hatimaye kupoteza fahamu na baadaye walipakiwa kwenye gari la Marwa kisha kusukumizwa korongoni.

Alisema baada ya kufanyiwa kitendo hicho, watuhumiwa waliwabeba Marwa na mwanawe hadi karibu na kituo cha mafuta ambako taarifa zilianza kuenea.

Watuhumiwa hao ambao pia ni wakazi wa Mtongani, Kunduchi mkoani Dar es Salaam, walikamatwa na askari na makachero walipofanya ukaguzi kwenye gari hilo, walibaini kuwemo na sindano zinazodaiwa kuwa za dawa za kulevya zinazohofiwa kuwa Marwa na John walichomwa.

Kamanda Chilya alisema Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watuhumiwa wawili huku akibainisha kuwa miili ya marehemu imehifadhiwa katika chumba cha maiti Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, Songea ikisubiri kutambuliwa na ndugu na kufanyiwa uchunguzi zaidi na madaktari.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Charles Hinju, alithibitisha jana kupokea miili ya watu wawili ya jinsia moja ambao inadaiwa waliuawa kikatili katika kijiji cha Lilondo, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na imehifadhiwa katika chumba cha maiti.

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# 'Mke wa Bilionea Msuya alikuwa na ugomvi wa mali na wifi yake'

**Na Grace Gurisha**



MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, amedai mahakamani kuwa Miriam Mrita, mke wa mfanyabiashara wa madini, marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', alikuwa na ugomvi wa mali na wifi yake, marehemu Aneth Msuya kwa kuwa alianza kuuza mali.

SSP Mhanaya alidai hayo juzi mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akiulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, katika kesi ya mauaji ya mwaka 2018 inayomkabili Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela.

Baada ya madai hayo ya shahidi, Wakili Kibatala alitaka kujua mali ambazo mteja wake (Mrita) alianza kuziuza na kubadilisha umiliki kutoka jina la marehemu mumewe kwenda jina la mtuhumiwa.

Kibatala: Shahidi, hebu ieleze mahakama maneno ambayo unadai kuwa Getruda alikwambia kuwa alimsikia mtuhumiwa anayatamka kuwa unayatafsiri vipi? Maneno yenyewe ni haya "Mali nitafute mimi, watumie wengine". Hii unaitafsiri vipi wewe mpelelezi uliyepata mafunzo kutoka kwa FBI Marekani?

**Shahidi:** Maneno haya yanaonesha kabisa kulikuwa na chuki za mali na kwa tafsiri yangu ni kwamba, kulikuwa na ugomvi wa mali kati ya marehemu Aneth na Mrita.

**Kibatala:** Ooh ugomvi wa mali eeh! Sasa hii unaithibitishaje? Iweke vizuri ili jaji na Wazee wa Baraza waweze kurekodi vizuri.

**Shahidi:** Kwa sababu tuliona mtuhumiwa wa kwanza (Miriam) ameanza kuuza mali.

**Kibatala:** Ukimwona Mheshimiwa Jaji, amemaliza kuandika, ieleze mahakama ni mali gani hizo ambazo walikuwa wanagombania marehemu na Miriam?

**Shahidi:** Tulianza kuona baadhi ya magari yalikuwa yameanza kubadilishwa majina.

**Kibatala:** Taja gari na namba zake.

**Shahidi:** Toyota Landcruiser ndiyo ilikuwa imebadilishwa jina.

**Kibatala:** Namba za gari?

**Shahidi:** Sizikumbuki, kwa sababu ni muda mrefu sana umepita.

**Kibatala:** Haya hukumbuki! Haya, tuambie kubadili umiliki kutoka kwa nani kwenda kwa nani?

**Shahidi:** Kutoka kwa Erasto Msuya, kwenda kwa Miriam Steven Mrita.

**Kibatala:** Kama akifariki mkewe, anaweza kubadilisha umiliki wa magari?

**Shahidi:** Hapo sasa tufanye uchunguzi.

**Kibatala:** Khee! We shahidi, mimi tena wakili ndiyo nifanye uchunguzi, siyo wewe tena?

**Shahidi:** (Kimya)

**Kibatala:** Wewe kama mpelelezi na SSP katika uchunguzi wako, ulishawahi kwenda TRA kujua umiliki huo ulihama vipi kutoka kwa Msuya kwenda kwa Mrita?

**Shahidi:** Huko TRA sikwenda, ila kuna askari wengine walikwenda kuchunguza hilo.

**Kibatala:** Shahidi, kwa ufahamu wako, huyu Getruda alipokamatwa huko, alifanyiwa upekuzi?

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, anayefanyiwa upekuzi ni mtuhumiwa.

**Kibatala:** Alifanyiwa?

**Shahidi:** Hakufanyiwa!

**Kibatala:** Ulipomfanyia mahojiano, ulijiridhisha kuwa alikuwa na simu au hakuwa nayo?

Shahidi: Hakuwa na simu.

Kibatala: Getruda akikusimulia kuwa alikuwa na simu na alipewa na washtakiwa na akaambiwa aitupe baharini, hii ni taarifa kutoka kwa mtu, anaweza hata akadanganya. Hii taarifa wewe uliithibitisha vipi?

**Shahidi:** 'Tuli-verify' (tulithibitisha).

**Kibatala:** 'Mli-verify' vipi?

**Shahidi:** Tuliwakabidhi wenzetu wa 'cybercrime' (askari wapelelezi wa makosa ya mtandaoni).

**Kibatala:** Wewe 'ulii-verify' vipi?

**Shahidi:** Tulikwenda naye hadi Feri, akatwambia kuwa alitumbukiza hapa.

**Kibatala:** Wewe kama Ofisa wa Polisi Mwandamizi, una taarifa nyingine ya kisayansi kwamba simu ilitumbukizwa hapo?

**Shahidi:** Tuliongea na wenzetu wa TEMESA wakasema simu ilitumbukizwa hapo, bahari haiwezi kutunza kitu, inaweza kutokea hata Comoro.

**Kibatala:** Kwahiyo, kwa ufupi hakuna?

**Shahidi:** (Kimya)

**Kibatala:** Uliweza kuchunguza iwapo marehemu Aneth Msuya, alikuwa na ugomvi na watu wengine kazini au sehemu yoyote?

**Shahidi:** Tuliweza kuwahoji watu mbalimbali, lakini hatukuweza kubaini.

**Kibatala:** Ulimhoji nani na nani kazini kwa marehemu?

**Shahidi:** Tuliwahoji watu mbalimbali hatukubaini.

**Jaji:** (akaingilia kati) Umeelewa swali lake?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kibatala:** Sasa mlimhoji nani na nani kazini kwa Aneth?

**Shahidi:** Mimi binafsi sikumhoji mtu yeyote.

**Kibatala:** Unafahamu kama Aneth alikuwa na mtoto wa miaka minne?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kibatala:** Ulimwambia Jaji kuwa mlipata kumhoji huyo mtoto?

**Shahidi:** Huyo mtoto nilimzungumzia kwenye maelezo yangu.

**Kibatala:** Mlimhoji?

**Shahidi:** Sikumbuki.

**Kibatala:** Sasa tukio lilifanyika ndani ya nyumba na mlisimuliwa na Getruda ambaye hakuwapo. Mlimhoji yule mtoto, maana mtoto wa miaka minne anaweza kueleza mambo?

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, hilo halikufanyika, kwa sababu yule mtoto alikuwa amelala.

Alipoamka ndipo akamwamsha mama yake bila kuamka, akaenda kwa mama muuza vitumbua, akamwambia anamwamsha mama yake haamki na amechafuka.

**Kibatala:** Huyo mama muuza vitumbua wewe ulimhoji?

**Shahidi:** Sikumhoji.

**Kibatala:** Wewe unamfahamu hata jina huyo mama muuza vitumbua?

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, Wakili ananiuliza mambo ambayo sikuwapo!

**Jaji:** (akaingilia tena) Shahidi umeulizwa unamfahamu?

**Shahidi:** Simfahamu.

Kibatala: Kwa taarifa zako, mwili wa marehemu ulikutwa wapi?

**Shahidi:** Kwenye korido.

**Kibatala:** Hiyo taarifa mpya. Sasa soma hii nyaraka.

**Shahidi:** Kwanza hii nyaraka nimeshaikataa tangu mwanzo.

**Kibatala:** Shahidi hii ni 'document' (nyaraka) ya mahakama, nimeiomba mahakamani, huwezi kuikataa. Kwa mujibu wa 'document' hiyo, mwili wa marehemu ulikutwa wapi? Soma hiyo 'document'!

**Shahidi:** Nimesema hii nimeikataa tangu awali!

Jaji: (akaingia kati tena) Shahidi wewe jibu swali!

**Shahidi:** (Anasoma nyaraka) Mwili wa marehemu ulikutwa chumba cha watoto, ukiwa umelala sakafuni, ukiwa uchi.

**Kibatala:** Hilo gari la Ford Ranger, wewe kama mpelelezi, unafahamu limesajiliwa kwa jina la nani?

**Shahidi:** Sikumbuki Mheshimiwa Jaji!

**Kibatala:** Unafahamu kuwa gari hilo lilipelekwa CMC Cooper Motors Company kwa matengenezo?

**Shahidi:** Sifahamu.

**Kibatala:** Na wewe mpelelezi, huyu mshtakiwa wa kwanza alifikia hoteli gani Dar?

**Shahidi:** De France Hotel.

**Kibatala:** Ambako kuna CCTV camera, siyo?

**Shahidi:** Ndiyo, lakini uwezo wa kuhifadhi taarifa yake ni ndogo.

Kibatala: Kwahiyo, hatuwezi kupata taarifa kuwa washtakiwa walifika hapo na gari gani, kwa kuwa 'storage' (uwezo wa hifadhi) ya CCTV ni ndogo?

**Shahidi:** Ndio, hatuwezi kupata video za picha, lakini mashahidi wapo waliompokea na wanaweza kueleza walimpa chumba gani.

**Kibatala:** Sawa, kama wapo kwenye orodha tutawauliza. Wakati unaongozwa, ulimwambia Jaji kwamba kuna shahidi aliyewapokea?

**Shahidi:** Watakuja kuizungumzia wengine.

**Kibatala:** Huyo shahidi aliyewapokea ni wewe uliyemhoji?

**Shahidi:** Ni wapelelezi wenzangu.

**Kibatala:** Ulipokwenda kumpekua mshtakiwa wa kwanza, uliwahi kuwauliza ndugu au watoto wake au 'housegirl' (dada wa kazi) kujiridhisha kama tarehe hiyo hakuwapo, alikuwa Dar?

**Shahidi:** Sikuona sababu, hao ni ndugu wangeweza kumlinda.

**Kibata:** Shahidi, wewe ndio 'uliji-introduce' (ulijitambulisha) kwenye record (kumbukumbu) kwamba ulifundishwa na FBI (Shirika la Upelelezi la Marekani), unafahamu kwanini hizo taasisi huwa zinafanya upelelezi kwa muda mrefu?

**Shahidi:** Sijui unataka 'kuachieve' (kupata) nini? Maana siwezi kuizungumzia taasisi ya nchi nyingine.

**Kibatala:** Ni wewe uliyetaja na huwezi kunipangia maswali! (anacharuka)

**Jaji:** (akaingilia tena) Shahidi, nimeshakwambia wewe jibu kama unavyoulizwa. Unafahamu au hufahamu?

**Kibatala:** Kwanini huwa wanachukua muda mrefu, miaka mitatu au zaidi kupeleleza kesi badala ya 'ku- rush' (kuharakisha)?

**Shahidi:** Kwa sababu wanahitaji umakini.

**Kibatala:** Sasa shahidi hapo namna yeye alivyofanya upelelezi, kuna umakini?

**Shahidi:** Usinifundishe wakili msomi!

**Kibatala:** Shahidi sijakufundisha, ni wewe umetaja kuwa ni kuwa na umakini, sasa ninakuuliza kuna umakini hapo?

**Shahidi:** Wakati mwingine kunakuwa na umakini.

Kutokana na Wazee wa Baraza kuwa washiriki kwenye kesi nyingine ya mauji ambayo ni ya mwaka 2012, Jaji Kakolaki aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 4 mwaka huu, itakapoendelea.

Katika kesi hiyo, Miriam Mrita ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshitakiwa mwingine ni Revocatus Muyela.

HABARI KITAIFA

# PSSSF ilivyoongeza thamani uwekezaji miaka mitano

**Na Jenifer Gilla**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kwa kipindi cha miaka mitano umeongeza thamani ya uwekezaji kutoka Sh. trilioni 6.40 hadi trilioni 7.92.

Mkurugenzi wa mfuko huo, Hosea Kashimba, alisema pia thamani yake imeongezeka kutoka Sh. trilioni 5.83 hadi Sh. trilioni 8.07 sawa na asilimia 27 ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 6.73 kwa mwaka.

Mfuko huo ulianzishwa mwaka 2018 baada ya kuuganishwa mifuko minne ya jamii ikiwamo ya Watumishi wa Mikataba Maalum (GEPF), Watumishi wa Serikali (LAPF), Watumishi wa Mashirika ya Umma na Kampuni Binafsi (PPF) na Watumishi wa Serikali Kuu (PSPF).

Kashimba alisema kutokana na mafanikio hayo wamelipa madai ya Sh. trilioni 1.03 yaliyorithiwa kutoka kwenye mifuko iliyounganishwa kwa wanufaika 10,273 ndani ya miaka miwili huku mfuko ukiendelea kulipa madai mapya. Kadhalika, mfuko umelipa jumla ya Sh. trilioni 8.88 kwa wanufaika 262,095, kwa wakati pensheni ya Sh. bilioni 67 kila mwezi, likiwa ni ongezeko la asilimia 100 ikilinganishwa na wastani wa Sh. bilioni 34 wakati mfuko huo unaunganishwa.

Kashimba alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitoa taarifa za utekelezaji wa mfuko huo kwa wahariri wa vyombo vya habari na kuongeza kuwa kupitia muunganiko wa mifuko hiyo wamepunguza muda wa kusubiri mafao wa wastaafu kutoka miaka mitatu hadi siku 60.

"Vilevile tumeboresha huduma za wateja na sasa tunatumia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), iliyovumbuliwa, kutengenezwa na kuendeshwa na wataalamu wa ndani kwa asilimia 90," alisema Kashimba.

Alisema mafanikio hayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na serikali kwa kutoa msaada wa hali na mali ikiwamo kulipa deni la Sh. trilioni 4.6 la wanachama wa uliokuwa Mfuko wa PSPF kabla ya mwaka 1999, hali iliyosababisha mfuko huo kulipwa Sh. trilioni 2.17 kupitia hatifungani maalum.

Pia, serikali ililipa Sh. bilioni 500 kati ya bilioni 731.4 deni la mikopo ya miradi ambayo mifuko iliyounganishwa iliikopesha serikali kutekeleza miradi yake ikiwamo ujenzi wa jengo la Bunge, Chuo cha Serikali cha Hombolo na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mfuko umeongeza vyanzo vya mapato kupitia uwekezaji ikiwamo kujenga majengo ya kukodisha ofisi na makazi ya watu katika mikoa mbalimbali nchini, Dar es Salaam na Dodoma.

Mfuko umeweka hisa katika kampuni zinazofanya vizuri kibiashara nchini ikiwamo benki ya CRDB, NMB, kampuni ya Swiss port, Tanga Cement na Tanzania Breweries (TBL).

Alisema tangu kuanzishwa mfuko huo umeandikisha wanachama wapya 140,162 na mwaka huu wanatarajia kuandikisha wanachama wapya takribani 40,000. Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kulipa deni la Sh. trilioni 4.6 lililoshindikana kwa zaidi ya miaka 20 hali iliyochangia kuongeza ukwasi na utendaji wa mfuko huo.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi (kushoto), akiteta jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kapteni mstaafu George Mkuchika, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# EWURA kuendelea kuratibu mabadiliko sekta umeme

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha kuwa inachangia kuleta maendeleo ya kiuchumi kitaifa, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati nchini (EWURA), imeendelea kuratibu mabadiliko katika sekta ndogo ya umeme (ESI) ambayo yanalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji kufikia megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Vilevile, imeboresha huduma za utoaji leseni za umeme kwa kuimarisha mfumo wa uombaji leseni kwa njia ya mtandao yaani LOIS, upangaji wa bei pamoja na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa ili kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti.

Aidha, inaendelea kukabiliana na mafundi umeme wasiyo na leseni kwa kutoa onyo na tahadhari kwa mafundi umeme wote wanaofanya shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme, bila kuwa na leseni hai iliyotolewa na mamlaka hiyo kuacha mara moja na kuomba leseni itakayo waruhusu kufanya shughuli hizo.

Kwa mujibu wa sheria ya umeme, kazi zote za ufungaji umeme, ikiwemo upanuzi, kubadili, kufanya marekebisho na matengenezo kwenye mifumo, zinatakiwa zifanywe na mafundi wenye leseni iliyotolewa na EWURA ili kuhakikisha shughuli hizo zinaendeshwa na watu wenye utaalamu stahiki kwa usalama wa watu na mali zao.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Titus Kaguo, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kuendesha shughuli hizo bila leseni atatozwa faini ya Shilingi milioni tano au kifungo cha miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja.

Alisema mpaka sasa mamlaka hiyo ilitoa leseni zaidi ya 6,000 kwa mafundi umeme Tanzania Bara, na kwamba ni kosa kisheria kufanya shughuli za ufungaji umeme bila kuwa na leseni ya EWURA.

Aidha, alisema mamlaka hiyo imeongeza juhudi kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi na Ushirikiano wa Umma na Sekta Binafsi (PPPs) na mtaji wa rasilimali watu ikiwa ni pamoja na ukuzaji wa wafanyakazi, ushiriki wao, kuzingatia utamaduni wa taasisi, kuajiri, kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

Pia, alisema mamlaka hiyo inaipa kipaumbele ufadhili wa kifedha ili kupanua shughuli za kifedha na kuipa nguvu ya kiuchumi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya EWURA, Sura ya 414.

Vilevile, alisema inatoa elimu kuhusu utekelezaji wa majukumu yake na uhamasishaji kwa umma, viongozi wa serikali na wadau wengine ili wajue na kushiriki katika mchakato wa kusimamia sekta za nishati na maji. "Programu hii imeanzia katika mikoa yote ya Kanda ya Ziwa kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Ofisi ya EWURA ya Kanda ya Ziwa inahudumia mikoa saba ambayo ni Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera, Geita, Simiyu na Kigoma," alisema.

Alisema elimu hiyo hutolewa kwa njia mbalimbali za mawasiliano ikiwamo luninga, magazeti, redio na mitandao. Hata hivyo, pamoja na kutumia njia hizo zote za mawasiliano wanatoa elimu kwa njia ya ana kwa ana kwa wananchi. Katika kuimarisha utoaji huduma za maji na usafi wa mazingira kwa wananchi, Kaguo alisema EWURA imekuwa ikikutana na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuhakiki taarifa zao za utekelezaji wa majukumu ili kuiwezesha kuandaa taarifa ya utendaji kazi wa mamlaka.

Kaguo alisema EWURA inashirikiana na vyombo vya habari kufikisha taarifa muhimu kwa wananchi hao kwa kuwa ni moja kati ya njia rahisi ya kuifikia jamii.

# Daktari feki akamatwa Muhimbili

**Na Anjella Mndolwa,** TUDARCo

MKAZI wa Mbagala Sabasaba, wilayani Temeke, Dar es Salaam, Mussa Mawa, amekamatwa katika maeneo ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akidaiwa kujihusisha kutapeli wananchi wanaopata huduma maeneo hayo kwa kujifanya daktari.

Inadaiwa Mawa alikuwa anajifanya daktari katika hospitali hiyo ili kupata riziki kutokana na ugumu wa maisha alionao.

"Leo (juzi) nina siku ya sita toka nimeanza kutapeli hospitalini hapa. Nilikuwa ninajifanya daktari na kumtapeli mama ambaye anamwuguza mgonjwa wake ambaye amelazwa wodi Na. 3 Mwaisela," alidai Mussa alipokamatwa hospitalini huko.

Ndugu wa mgonjwa, Sada Ramadhani, alisema kuwa mama yake amelazwa Mwaisela katika chumba cha uangalizi maalum (High Dependant Unit). Tapeli huyo alimwambia kuwa mgonjwa wake amezidiwa na anatakiwa apatiwe huduma za haraka ili apone.

"Aliniambia 'ili mgonjwa wako apone unatakiwa kutoa kiasi cha Sh. 140,000 tumpatie matibabu ya haraka'. Nilikuwa katika harakati za kutoa hiyo fedha na tukiwa kwenye maongezi, alikuja mlinzi alitukuta na alipomhoji alibaini ni tapeli," alisema Sada.

Mkuu wa Idara ya Ulinzi MNH, Alfred Mwaluko, alisema walimbaini kuwa ni daktari feki maeneo ya chumba cha kuhifadhi maiti, akiwa katika harakati za kuwatapeli wananchi wanaouguza ndugu yao aliyelazwa Mwaisela.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, alitoa rai kwa wananchi wanaojihusisha na kutapeli wananchi wengine katika eneo la hospitali hiyo, kuacha mara moja kwa kuwa ulinzi umeimarishwa na wakijaribu kufanya hivyo watakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya usalama.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wateule wapya wa Rais Samia watekeleze wajibu kwa viwango

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri kwa lengo la kuimarisha utendaji serikalini. Katika mabadiliko hayo, Rais alianzisha nafasi ya Naibu Waziri Mkuu ambaye kazi yake kubwa itakuwa kuratibu shughuli za serikali.

Mbali na kuanzisha nafasi hiyo na kumteua Dk. Dotto Biteko kushika wadhifa huo, ambaye pia atakuwa Waziri wa Nishati, Rais pia alivunja Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kuunda mbili, moja ikibeba dhamana ya ujenzi na nyingine uchukuzi. Pia aliimarisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuwa na Naibu Waziri na mtendaji kwa ajili ya masuala ya Afrika Mashariki.

Sambamba na mabadiliko hayo, Rais Samia aliwateua mawaziri wapya katika baadhi ya wizara kwa kuwapandisha kutoka naibu mawaziri au kwa kuwateua kutoka miongoni mwa wabunge na kuwateua naibu mawaziri wapya. Pia aliwahamisha mawaziri kutoka wizara moja kwenda nyingine pamoja na kuwatema waziri mmoja na naibu mawaziri wawili waliokuwapo awali.

Vilevile, Rais alifanya mabadiliko ya makatibu wakuu wa wizara kwa kuwapandisha kutoka unaibu makatibu wakuu na wengine kutoka kwenye utumishi na pia kuwateua naibu makatibu wakuu wapya. Wengine walihamishwa kutoka katika wizara moja kwenda nyingine.

Kutokana na mabadiliko hayo, watu mbalimbali wamepongeza huku wakiweka bayana kwamba yana lengo la kuimarisha utendaji katika serikali pamoja na kuongeza kiwango cha uwajibikaji miongoni mwa wateule hao.

Wateule hao wa Rais, wakiwamo walioteuliwa kwa mara ya kwanza, kupandishwa na kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine, watambue kuwa hawakupewa nafasi hizo kwa bahati mbaya wala upendeleo bali ni kutokana na maoni ya Rais pamoja na ushauri aliopewa na wasaidizi wake kuwa nani anafaa kuwa wapi ili kuhakikisha utendaji kazi serikalini unakuwa wa viwango.

Dhamira ya Rais inajulikana wazi kuwa wananchi wapate huduma zinazostahili na kwa viwango, hivyo wateule hao wanapaswa kutekeleza majukumu hayo kama ambavyo aliyewateua anataka. Kwa maneno mengine, mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu walioteuliwa au kuhamishwa wizara, wanatakiwa kutoa huduma bila upendeleo wala huba kama ilivyo kwenye viapo vyao.


Kwa wale ambao wanaingia katika wizara ambazo wenzao wametemwa au kuhamishwa, wanapaswa kujifunza kuwa kama viatu wanavyovaa katika nafasi hizo vitawapwaya, hawataonewa huruma pindi hali itakavyokuwa hivyo. Pia wanatakiwa kujifunza kwa nini wenzao hao wameondolewa na wao kupelekwa katika wizara hizo. Hilo linapaswa kuwa dira kwao na kuchambua kwa undani kwamba mahali hapo si salama kwa mtu yeyote atakayefanya ndivyo sivyo.

Kuna msemo kwamba ukiaminiwa katika nafasi yoyote au katika jambo fulani, mwonyeshe yule aliyekuamini kwamba unaweza. Kwa mantiki hiyo, wateule hao wa Rais, watambue kuwa wameaminiwa na aliyewateua kuwa wana uwezo, hivyo hawana budi kuonyesha kuwa wana uwezo kwa kutekeleza majukumu yao kwa viwango vya hali ya juu na kwa uaminifu.

Sambamba na hilo, viongozi hao walioteuliwa watambue kwamba wamepewa nafasi hizo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kulingana na sekta wanazoziongoza, hivyo watoe huduma na wananchi watatuliwe kero zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Julieth Ng'oma, SJMC

# Vijana kuhamasishwa kujiunga na vyuo ufundi, ajenda muhimu kwao na serikalini

**MARA** zote serikali , imekuwa ikitoa kipaumbaule katika kuongeza uwekezaji wa vyuo vya ufundi, ili kuwapa fursa vijana wengi kujifunza kwa vitendo na kuendeleza stadi za maisha kwenye mafunzo kama ufundi wa umeme, magari, bomba na ujuzi mwingine.

Pia, serikali ilisema imetenga kiasi cha bilioni 100 kwa ajili ya kutengeneza vyuo 64 kwenye wilaya, zilizokuwa hazijajengwa vyuo hivyo lengo kuu likiwa kupunguza vijana wasio na ajira na kuwapa ujuzi utakaowasaidia kujiajiri wenyewe.

Aidha mashirika mbalimbali na serikali yamekuwa yakisaidiana kutoa ufadhili na mikopo kwa vijana wasio na uwezo kugharamia masomo yao, ili kusiwapo kisingizio kinachomkwamisha kijana kujiunga na masomo hayo.

Kutokana na juhudi hizi zilizofanywa na serikali na mashirika ya kusaidia vijana jinsi yanavyojitoa kuhakikisha wanapata maarifa, basi vijana wanatakiwa kuwekeza nguvu na akili zao katika kujifunza ili kupata matunda ambayo yataleta faida kwa Taifa.

Fursa hizo zilizotolewa kwa vijana, wanatakiwa kuzichangamkia kwa ajili ya manufaa yao na nchi kwani endapo kutakuwa na mwamko wa kujiunga katika kupata ujuzi na maarifa kwa njia ya vitendo itachangia ukuzaji wa uchumi nchini.

Vijana hao wanaweza kujifunza ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na kuwa na uwezo wa kujitegemea, kwa kufanya kazi za ufundi watakazochagua kujifunza.

Baada ya kupata ujuzi huo na kuweza kujitegemea, inawafanya kupunguza kasi ya utegemezi, ambao umekuwa kikwazo kikubwa katika familia nyingi, kwani kijana anapokosa kazi ya kufanya, anaamua kuendelea kuishi kwa wazazi kwa kuogopa ugumu wa maisha.

Vilevile vijana wa mitaani wanapaswa kushauriwa kujiunga na mafunzo ya ufundi, kwani hiyo itasaidia kupunguza ongezeko la uhalifu na vijana wanaozurura bila ya kuwa na ujuzi wowote.

Endapo wengi wao watapata nafasi za kujifunza tutaweza kuwa na wajasiriamali wabobezi, ambao wataweza kupata fursa mbalimbali za ajira na kupitia wao tutaweza kujua misingi madhubuti ya uzalishaji wa bidhaa na uwezo wa kutafuta soko la kuuzia bidhaa hizo.

Kunapokuwapo wajuzi wengi nchini, hiyo inakuwa njia itakayochangia ongezeko la ajira, kwani kila mmoja atakuwa na uwezo wa kujiajiri na kupunguza kasi ya uhaba wa ajira nchini.

Mafanikio ya taifa sasa yanawategemea vijana, kwani ndio wenye wajibu na uwezo zaidi wa kujenga jamii, kwa sababu wana nafasi kubwa ya kuepusha hatari na changamoto zinazokabili utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

Wengi wanapaswa kuwa na nguvu za hoja zenye mashiko ambazo zinaweza kulitetea kwa kudadavua na kuzungumzia maslahi ya nchi yao.

Vijana wanapewa kipaumbele kwa sababu wao ni tofauti na watu wazima kwani wanaweza kufikiri na kutenda kwa haraka kutokana na nguvu walizo nayo, hivyo sio vyema kushiriki vitendo vinavyochochea uhalifu au vurugu.

Taifa lolote lililoendelea na linaloendelea linahitaji vijana wenye nguvu, akili, heshima, fikra chanya na wenye uzalendo na nchi yao kukubali kutumika katika kukuza na kuendeleza vile vyote vilivyoanzishwa.

Kwa sababu, endapo kutakuwa na vijana wenye fikra chanya watakuwa tayari kupambana kwa ajili yao na vizazi vyao vijavyo, na kukamilisha ajenda ya mwaka 2030 kwa ajili ya maendeleo endelevu.



Mmoja wa watoto wenye ulemavu akisokota nyuzi kwa mashine maalum kwa ajili ya kushona vikoi katika kituo cha mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali cha umoja wa wanawake wa Ifakara IWWA. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Serikali yashauriwa kuanzisha programu vyuo vya ufundi kusaidia vijana wenye ulemavu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

SERIKALI imeshauriwa kuanzisha programu maalum kwenye vyuo vya ufundi na vya maendeleo ya jamii kuwezesha vijana wenye ulemavu wa akili kujifunza ufundi na kuwa na fursa za kujiajiri au kuajiriwa sawa na wengine.

Ushauri huo umetolewa Ifakara wilayani Kilombero, mkoani Morogoro na Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Mafiga Women and Youth Development Organisation (MWAYODEO), Venace Mlali, alipotembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Ifakara na Umoja wa Wanawake Ifakara (IWWA) na kuona wanavyotoa mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali kwa vijana wenye ulemavu wa akili.

Alisema kwa kushirikiana na Shirika la Vaasa Tanzania Association nchini Finland, wameanzisha mradi wa kuhamasisha vijana wenye ulemavu wa akili kupata stadi za ufundi kwenye vyuo vya Serikali vya Maendeleo ya wananchi (FDC) na VETA ili kuwawezesha kupata ujuzi kupitia fani mbalimbali.

"Nia ni kuhakikisha wanaweza kujitegemea, tunahakikisha wanapata ujuzi na stadi kwenye ufundi wa ujenzi, kufyatua matofali, ufundi bomba, ushonaji, useremala na upishi," alisema Mlali.

Alisema ni vyema kwa jamii hususani wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu wakatambua kuwa kundi hilo lina nafasi ya kujifunza na kupata fursa za kujiajiri ama kuajiriwa kama walivyo vijana wengine na kudumu kuendesha maisha yao kama watasaidika.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, waliwafikia vijana 150 wenye ulemavu wa akili na kati yao 21 wamepata mafunzo kwenye chuo FDC.

"Mradi huu umekuwa chachu kubwa ya kuwaibua vijana wenye ulemavu wa akili lengo kubwa ni kuwawezesha kuboresha maisha yao na familia yao, tumebaini pia vijana hawa wanaweza kufundishika, kwa muda mfupi waliopata mafunzo na stadi mbalimbali wameonesha mafanikio ya kuzitumia hivyo watahamasisha wadau zaidi ikiwamo serikali kuona namna bora zaidi kuwasaidia wengine," alisema.

Pia kuwa na mfumo imara wa mawasiliano kuanzia kwenye jamii, wazazi walezi na walimu wa vitengo maalumu kwenye shule za msingi na vyuo ili vijana hao wenye ulemavu waweze kujiunga kwa wakati na kwamba kwa sasa vyuo vingi vya ufundi havina walimu wenye ujuzi wa kufundisha vijana wenye ulemavu wa akili.

Mmoja wa walimu wa fani ya ushonaji FDC Ifakara, Leah Kipambe, alisema wanafunzi hao wamekuwa na uelewa mkubwa wakifundishwa licha ya changamoto ya kusahau mara kwa mara na wakiendelea kufundishwa zaidi kunaweza kuwa na mabadiliko.

Mkuu wa FDC Ifakara, Dolorosa Mhagama, alisema kwa sasa wana wanafunzi 21 wenye mahitaji maalumu wanaosoma fani tano na licha ya changamoto kadhaa bado wamekuwa na uelewa tofauti na walivyoanza mafunzo chuoni hapo.

Alisema wamekuwa wakiwachanganya wanafunzi hao na wengine wa kawaida wa mafunzo jumuishi hali inayofanya kubadilika kwa haraka.

"Hata hivyo muda wao wa kujifunza umekuwa ni mfupi mdogo sana, angalau serikali ingeungana na wadau hawa wa maendeleo kutoka sekta binafsi ili vijana hawa wapate muda mrefu zaidi wa kujifunza," alisema.

Aliwaasa wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu kujifunza chuoni hapo ili wapate stadi na kujiajiri au kuajiriwa na kuacha kuendelea kuwafungia majumbani bila msaada na wengine kuwageuza ombaomba.

## Wawili mbaroni tuhuma za kudanganya mtu amedondoka kwa usafiri wa ungo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linawashikilia watu wawili kwa mahojiano kwa kutoa taarifa za uongo kuwa kuna mtu amedondoka kanisani kwao akiwa anasafiri kwa ungo unaodaiwa kuwa ni wa kishirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema Agost 24 katika kituo cha Polisi Kibaha, Mchungaji wa Kanisa la Pentecostal Gospel Mission, Emmanuel Paul, alitoa taarifa za Basenga Silvester (59), mkazi wa Miswe kudondoka kanisani akiwa anasafiri kwa ungo wa kishirikina na kuleta taharuki kwa waumini.

Kamanda Lutumo alisema siku ya tukio kulikuwa na ibada ya mkesha na mtuhumiwa akiwa na wenzake sita ambaye anadaiwa kudondoshwa kwa sala na maombi ya waumini na mchungaji na kufanikiwa kutoroka kichawi.

"Kwa mujibu wa taarifa zilizofika kituoni mchungaji wa kanisa hilo alimchukua mtu huyo akiwa na vifaa vyake vya kishirikina na kumuweka ofisini hadi asubuhi polisi walipofika kumchukua," alisema Kamanda Lutumo.

Lutumo alisema katika uchunguzi uliofanywa na jeshi hilo, ulibaini tukio hilo lilikuwa la kutengeneza, kuwalaghai na kuwahadaa waumini ili kujiongezea waumini zaidi.

Imeelezwa kwamba Basenga alijinasibu kuwa yeye na wenzake walifika kanisani hapo kishirikina kwa lengo la kuwapima imani waumini na kwamba mtuhumiwa aliahidiwa kulipwa Sh. 50,000, baada ya kufanya ulaghai huo.

Polisi mkoani Pwani imetoa onyo kwa watu wenye tamaa ya kujipatia kipato cha haraka kwa kufanya ulaghai kuacha mara moja.

KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Faini mil 5/- abiria wa basi 'akichimba dawa'

## -Ukitoa ushahidi wa picha una zawadi yako NEMC

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeonya mabasi yanayosimama njiani kwa ajili ya abiria kuchimba dawa. Watakabiliwa na faini ya hadi Sh. milioni tano.

Hata hivyo, NEMC imesema kuwa kabla ya kuanza kutoa faini hizo, itaendesha kampeni ya elimu kwa umma kwa kipindi cha mwezi mzima kuanzia mwezi huu kwa wenye mabasi na baada ya hapo itaanza kuchukua hatua dhidi ya watakaokiuka sheria.

Jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, alitangaza hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni hiyo.

Alisema NEMC ina kanda 17 nchi nzima ambazo zitatumika kutoa elimu kwa wamiliki wa mabasi kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini na taasisi zinazohusika na usafiri wa nchi kavu.

"Mabasi nchi nzima yanafanya uchafuzi huu wa mazingira. Kwahiyo, kwanza tunataka kutoa elimu kwa sababu tukianza kuwatoza faini, watasema 'mbona hamkutuambia'. Kwahiyo, mwezi mzima wa tisa (Septemba) utakuwa wa kutoa elimu tu ," alisema Dk. Gwamaka.

Kuhusu kutupa taka nje ya mabasi, Mkurugenzi Mkuu huyo alisema elimu itatolewa kwa mabasi ya masafa marefu na daladala za mijini na maeneo watakayotoa elimu ni stendi zote. Alisema baada ya mwezi mmoja, wataanza kuchukua hatua kwa watakaosimamisha mabasi kuchimba dawa. Mwananchi atakayejitolea kupiga picha mabasi hayo atapata motisha kwa kazi hiyo.

"Mwananchi akiona basi limesimama watu wanajisaidia, piga picha namba za mabasi na ushahidi wa watu wanaojisaidia. Sisi huyo mwenye basi tutashughulika naye kwanza kwa kumpiga faini isiyopungua Sh. milioni tano na inaweza kuhusisha kumpokonya leseni ya kufanyabiashara hiyo.

"Kuanzia tarehe 2 Oktoba, hatutarajii kuona basi linasimama kwa ajili ya kuchimba dawa kwa sababu tutakuwa tumetoa elimu ya kutosha na atakayefanya hivyo atakuwa anakaidi tu kwa makusudi na ninawahakikishia kwamba tunamshughulikia atakayethubutu," alionya.

Dk. Gwamaka alisema kuwa mwezi Oktoba mwaka huu, NEMC itatangaza donge nono litakalotolewa kwa mwananchi ambaye atajitolea kupiga picha basi ambalo limesimama na abiria wake wakijisaidia.

Dk. Gwamaka alisema wafanyabiashara wa mabasi wanaonunua mabasi mapya ya kwenda mikoani, wanunue mabasi yenye vyoo ili kuwapunguzia matatizo abiria wanapotaka kwenda kujisaidia.

Aliwapongeza wamiliki wa baadhi ya mabasi yanayofanya safari zake kwenda mkoani Dodoma, Arusha na Mbeya ambao mabasi yao yana vyoo, hivyo kutochangia kuchafua mazingira kama yale yasiyo na vyoo ndani.

"Basi likiwa na choo ndani, abiria wanastarehe sana na wanakunywa maji kwa sababu wana uhakika wa kwenda chooni na kuwa na choo ndani siyo jambo la ajabu ambalo haliwezekani. Ni kwa sababu tu tulikuwa hatujalitilia mkazo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu huyo pia alisema wenye vituo vya mafuta wanaweza kusaidia kwa kujenga vyoo vingi ili wenye mabasi watumie kusimama na abiria wao kwenda kujisaidia badala ya kwenda porini.

# Marufuku kutumiana nyaraka za serikali kwa WhatsApp

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, ameonya utumaji wa nyaraka za serikali kwa njia zisizo rasmi ikiwamo WhatsApp, unakwenda kinyume cha sheria inayosimamia nyaraka za serikali.

Ridhiwani alitoa angalizo hilo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate, aliyehoji uhalali wa matumizi ya makundi ya Whatsaap kutumiana nyaraka.

"Sheria inaelekeza kuwa mawasiliano ya serikali yafanyike kwa njia ya barua na si vinginevyo na haitakuwa sawa, na ni marufuku kwa serikali kuwasilisha au kutumiana nyaraka kwa njia ya WhatsApp isipokuwa kwa maelekezo ambayo yatakuwa yametolewa vinginevyo katika mamlaka," alisema.

Naibu Waziri huyo alilihakikishia Bunge kuwa serikali inaendelea kutengeneza mifumo mbalimbali ambayo italeta serikali yote katika alichokiita adabu ya utendaji.

Awali katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini serikali itarekebisha sheria za utumishi zilizopitwa na wakati hasa kipindi hiki cha teknolojia.

Ridhiwani, akijibu swali hilo, alisema serikali ilitunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Na.10 ya Mwaka 2019 ili kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi wa serikali na imewezesha kusanifiwa na kujengwa jumla ya mifumo 860 ya TEHAMA serikalini.

Alisema serikali inatambua kuwapo maendeleo makubwa ya kiteknolojia ambayo yamekuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha utendaji kazi katika utumishi wa umma.

Ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, Naibu Waziri alisema serikali imeendelea kufanya mapitio ya mfumo wa kisheria unaosimamia utumishi wa umma nchini.

"Mwaka 2019, serikali ilitunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Na.10 ya Mwaka 2019 ili kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi wa Serikali," alisema.

Alifafanua kuwa kupitishwa sheria hiyo, kumeisaidia serikali kuboresha utendaji kazi wake kupitia matumizi ya teknolojia.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo (katikati), akikabidhi kitabu kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa kuanza kutoa hatifungani ya kijani yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 300 sawa na Sh. bilioni 780 kutoka Benki ya CRDB ambayo ni ya kwanza kutolewa Tanzania na ya kwanza kwa ukubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (watatu kulia), Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Prof. Neema Mori (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (watatu kushoto), Mwakilishi kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Robert Mshiu (wapili kushoto) na Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Mary Mniwasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatifungani ya kijani yaanza kuuzwa, waziri aipongeza CRDB rekodi mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, ameipongeza Benki ya CRDB kwa hatifungani yake ya kijani yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300 zitakazowekezwa katika miradi yenye mrengo wa kulinda mazingira.

Alitoa pongezi hizo jana alipozindua uuzaji wa hatifungani hiyo jijini Dar es Salaam, akihimiza Watanzania kuanzia mtu binafsi, kampuni, taasisi za kimataifa hata mashirika ya umma kuichangamkia.

"Hatifungani hii ni ya kihistoria siyo tu katika sekta ya fedha nchini, bali nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara. Benki ya CRDB inakuwa ya kwanza kuitoa.

"Ni hatifungani itakayowezesha kupata fedha za kutekeleza miradi ya kuhifadhi mazingira na yenye matokeo chanya kwa jamii yaani green, social and sustainability bond. Hatifungani hii pia ni ya kwanza kwa ukubwa kusini mwa Jangwa la Sahara. Hongereni sana Benki ya CRDB," alipongeza.

Waziri Mkumbo alisema kuuzwa kwa hatifungani hiyo, siyo tu ni mafanikio kwa Benki ya CRDB inayoingia katika historia ya kutoa hatifungani yenye thamani kubwa zaidi Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, bali Tanzania kwa ujumla.

"Mkifanikiwa kuuza hatifungani hii na mimi nitakuwa nimefanikiwa kwa kuwa nikienda kwa Mheshimiwa Rais kumpa ripoti ya uwekezaji, sitaacha kusema kuhusu hatifungani hii."

"Riba mnayotoa ya asilimia 10.25 ni kubwa na itawafaa wote watakaoinunua. Kama ambavyo sisi tunakwenda kujifunza kwa wenzetu kuhusu masuala tofauti yatakayotufaa, nao waje kujifunza kuhusu hatifungani ya kijani," alipongeza Waziri Mkumbo.

Uuzaji wa hatifungani hiyo, waziri huyo alisema ni hatua muhimu katika ustawi na maendeleo ya uchumi nchini kwa kuwa utachangia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa 2020/21 - 2029/30) wenye lengo la kuwezesha upatikanaji rasilimali fedha kwa ajili ya miradi katika sekta ya umma na binafsi ili kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu.

Akizungumza na mamia ya wawekezaji, waandishi wa habari na wageni waalikwa walojitokeza katika hafla ya uzinduzi wa uuzaji wa hatifungani hiyo utakaodumu mpaka Oktoba 6 mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema uamuzi wa kutoa hatifungani hiyo umetokana na mahitaji makubwa ya mikopo pamoja na mwelekeo wa dunia katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Athari za mabadiliko ya tabianchi zimezigusa jamii nyingi duniani, hivyo kulazimu kuunganisha nguvu za kukabiliana nazo. Mafuriko, ukame na mlipuko wa magonjwa ni baadhi ya matokeo ya mabadiliko haya ya hali ya hewa ambayo hatifungani ya kijani inakusudia kuwezesha miradi ya kukabiliana nayo.

"Nchi nyingi duniani zinatoa hatifungani hizi na sasa ni zamu yetu, hivyo ninamwomba kila Mtanzania kujitokeza kuwekeza ili kwa pamoja tuyalinde mazingira yetu," alisema Nsekela.

Hatifungani hiyo ya miaka mitano itauzwa kwa awamu, lakini kwa awamu ya kwanza Benki ya CRDB inakusudia kukusanya Sh. bilioni 55.

HABARI KANDA KASKAZINI



# Wilaya 15 zapewa bil.7/- utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MFUKO wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF), umeziwezesha wilaya 15 ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi rafiki na mazingira.

Lengo la miradi hiyo ni kuendelea kuhifadhi bioanuwai zinazopatikana ndani ya misitu iliyopo kwenye safu za milima hiyo.

Jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya EAMCE, Prof. John Kessy, alisema miradi inayotekelezwa ni zaidi ya 400.

Prof. Kessy, alikuwa akizungumza na wadau mbalimbali jijini Arusha, wakati wa mkutano wa 13 wa Shirikisho la Mifuko ya Uhifadhi wa Mazingira Barani Afrika.

Miradi hiyo ni pamoja na ya upandaji zaidi ya milioni 24 kwenye eneo la hekta 27,000 la Milima ya Tao la Mashariki.

Mingine iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa ni ufugaji wa mbuzi na maziwa 550, ng'ombe wa maziwa 100, kuku 15,000, nguruwe 800, ufugaji wa nyuki katika mizinga ya kisasa 1,400.

Imo pia, teknolojia ya matumzi ya majiko banifu kwenye kaya 15,000, uwekaji na uimarishaji wa mipaka ya misitu ya hifadhi kwenye zaidi ya kilomita 2,500 katika vijiji 130.

Kwa mujibu wa Prof. Kessy, utekelezaji wa miradi hiyo umekuwa na matokeo chanya kwa wananchi na misitu inayohifadhiwa, kwa kuwa wananchi walengwa, wengi wao ni wale wanaopakana na hifadhi za mazingira asili za Chome mkoani Kilimanjaro, Amani, Magamba na Nilo zilizopo Mkoa wa Tanga.

"Aidha matokeo hayo yanaonekana pia katika Hifadhi za Mazingira Asili ya Udzungwa Scarp, Kilombero, Mkingu, Uluguru na Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa inayopatikana kwenye mikoa ya Iringa na Morogoro.

...Huko wananchi wameweza kuongeza kipato na kuwa mabalozi wa uhifadhi wa misitu hiyo, ambayo kwa asilimia kubwa imerejesha uoto wake wa asili."


Kuhusu umuhimu wa misitu hiyo ya Milima ya Tao la Mashariki, Prof. Kessy, alisema ndio vyanzo vikuu vya maji kwa matumizi ya viwanda vikubwa nchini pamoja na wananchi wanaokadiriwa kufikia asilimia 25 ya Watanzania wote.

Misitu hiyo, pia inategemewa kwenye uzalishaji wa umeme nchini, ikizalisha zaidi ya asilimia 90 ya umeme wote unaozalishwa kwa nguvu za maji nchini.

Akizungumza kwenye mkutano huo wa Shirikisho la Mifuko ya Uhifadhi wa Mazingira Barani Afrika, Rais wa Shirikisho hilo, Dk. Theophile Zognou, alisema shirikisho hilo lilianzishwa rasmi nchini katika kikao cha kwanza kilichofanyika jijini Dar es Salaam, Septemba mwaka 2011.

Alisema lengo ni kuunganisha nguvu za pamoja kwenye uhifadhi wa rasilimali za misitu katika bara hilo, kwamba hadi kufikia sasa mfuko huo una wanachama 19, ikiwamo EAMCEF.

Dk. Zognou, alisema nguvu ya pamoja inahitajika kwa serikali zenye mifuko hiyo upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya uendelevu utakaowezesha kuendelea kutunza bioanuwai zilizopo na kuweka mazingira salama ya sayari ya dunia kwa vizazi vijavyo.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (wa tatu kulia), akijadiliana jambo na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Warda Abeid (wapili kushoto), katika mkutano wa kusikiliza kero na changamoto za wakazi wa Kijiji cha Lormorijoi, Kata ya Langai, juzi.
**PICHA: GIFT THADEY**

# Tatizo wanafunzi kusongamana darasani lapatiwa ufumbuzi

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

SHIRIKA la TES School in Africa la nchini Denmark, limetatua tatizo la muda mrefu la msongamano wa wanafunzi darasani, kukosa madawati uliokuwa ukizitesa shule za msingi Ambureni na Nkoanrua zilizoko Halmashauri ya Meru, mkoani Arusha.

Akizungumza jana, wilayani humo, wakati wa hafla ya kukabidhi samani hizo, Mratibu Mkazi wa shirika hilo Tanzania, Steven Ndossi alisema uamuzi wa kusaidia shule hizo, unalenga kuinua kiwango cha elimu shuleni.

"Leo tumekabidhi madawati, meza, viti na mbao za kisasa za kuandikia darasani, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi milioni 70. vifaa hivi vinaweza kutumiwa na wanafunzi 370 wa shule za msingi Ambureni na Nkoanrua.

"Nia yetu kwa ujumla ni kuwasaidia wanafunzi wa shule hizi kusoma katika mazingira mazuri na kuondoa msongamano darasani, uliosababishwa na uhaba wa meza na viti.

...Mwaka jana, TES School in Africa (Tanzania), ilitoa msaada wa jiko la kisasa la kupikia kwa Shule ya Sekondari Poli, kuweka umeme wa jua kwa shule za msingi Ambureni na Moivaro. Pia tulikabidhi samani za kisasa kwa Shule ya Sekondari Poli na Shule za Msingi za Ambureni na Moivaro."

Aidha, alisema lengo la shirika hilo ni kufikia shule nyingi kadri iwezekanavyo ili kupunguza ama kuondoa kabisa uhaba wa samani katika shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Shirika hilo lililoanzishwa mwaka 2014 huko Denmark, linajishughulisha na kutafuta marafiki wafadhili wa shule za msingi na sekondari ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi .

Aidha, alisema kwa mwaka ujao, wanatarajia kuleta samani mbalimbali kama vile kompyuta na LCD Projector kwa ajili ya Shule ya Sekondari Nkoanrua na Naurey Golden.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meru, Felister Nanyaro, akizungumza katika hafla hiyo, alipongeza shirika hilo kwa namna ambavyo wanaunga mkono serikali katika suala la elimu ambapo aliwaomba kuangalia namna ya kuzisaidia shule zilizopo pembezoni, ambazo zinakabiliwa na matatizo mbalimbali.

## Mwitikio wajawazito kwenda kliniki waongezeka Manyara

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MWITIKIO wa wajawazito na jamii za kifugaji zinazoishi Mkoa wa Manyara kwenda kliniki umeongezeka baada ya serikali kutoa taarifa inayoonyesha wajawazito 73,661 wamejitokeza katika kipindi kisichozidi miezi mitatu.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa mkoani humo, Emma Ngatoluwa, wanawake hao wamejitokeza kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

"Hao ni wale waliohudhuria kliniki katika kipindi cha robo mwaka ili waweze kupatiwa huduma ya afya na kulinda afya za watoto wao tumboni na kuwezesha kuendelea kukua vizuri," alisema.


Ngatoluwa, alisema mjamzito anapopata ujauzito, anatakiwa kuanza kliniki miezi mitatu ya kwanza au chini ya miezi hiyo.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho mahudhurio chini ya wiki 12 ni watu 6,102, mahudhurio ya zaidi ya wiki 12 ni watu 13,772, mahudhurio ya kwanza ni 19,874 na mahudhurio ya nne ni watu 21,710.

Kadhalika, alisema ili mjamzito aweze kutimiza mahudhurio yote ya kliniki wakati wa ujauzito inabidi ahudhurie mara nane Hadi anapojifungua.

Mratibu huyo, pamoja na mambo mengine, alisema mjamzito akianza mapema kliniki, inamsaidia kujua maendeleo yake, kwa kuwa akipimwa akakutwa hana damu ya kutosha anapewa dawa za kuongeza damu na dawa za madini chuma.

Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe mkoani Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema kwa mtu anayeshindwa kuhudhuria kliniki wanatumia Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 200, kumbana japo hawatumii nguvu kwa kuwa jamii inauelewa juu ya kliniki.





# Madiwani Tarime wakemea uvamizi maeneo ya hifadhi

**Na Timothy Itembe,**
MARA

MADIWANI wa Halmashauri ya Tarime Mjini wamekemea vitendo vya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya hifadhi na kuanza kufanya shughuli zao pamoja na kutaka kujimilikisha kinyume na sheria.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, ambaye ni Diwani Kata ya Nkende, Danieli Komote, alitoa kauli hiyo kwenye baraza la madiwani la robo ya nne akisema kuwa vitendo hivyo vinaiingizia hasara halmashauri na serikali.

"Tunatumia gharama kubwa kusuluhisha migogoro kwenye maeneo ya serikali yaliyovamiwa na baadhi ya watu na kufanya shuguli zao kama vile kujenga na shughuli zingine, hivyo nawaomba wananchi wetu ambao ni wapiga kura tusivamie maeneo yaliyotengwa ya serikali badala yake tuzingatie na kufuata sheria" alisema Komote.

Kadhalika, Mwenyekiti huyo aliitaka Idara ya ardhi kuzingatia sheria za ardhi zilizopo na kuacha tabia ya kuuza viwanja zaidi ya mara moja jambo ambalo linazua migogoro katika jamii.

Naye, Diwani wa Viti Maalumu, Doris Chacha alisema kuna baadhi ya watumishi wa ardhi ambao siyo waaminifu ambao wanatumia nafasi waliyonayo kuuza kiwanja kimoja kwa watu wengi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Gimbona Ntovya, alisema hadi sasa kesi nyingi za migogoro ya ardhi mahakamani na zingine wameanza kushinda, lakini wasingependa kuendelea kuwa na kesi hizo kwani kwa kiasi kikubwa wananchi ndiyo wanashindwa.

# Wazee Buchosa walia kunyimwa huduma za afya bure

**Elizabeth Seleman,**
BUCHOSA

BAADHI ya wazee kutoka Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza wameiomba serikali kuingilia kati suala la utolewaji wa huduma za afya bure kwao katika vituo vya afya na zahanati.

Wamesema kwa sasa wanaendelea kunyimwa huduma hizo katika vituo mbalimbali vya afya kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kutokuwa na vitambulisho.

Waliyasema hayo katika nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe na kueleza kuwa vitambulisho vinavyohitajika katika maeneo ya kutolea huduma bado havijatolewa na halmashauri, hali inayowasababisha wazee hao kukosa huduma zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Wakizungumza katika nyakati tofauti, Leah Salingu (80), aliieleza Nipashe kuwa wazee wanaendelea kuteseka pindi wanapoenda kupatiwa huduma kwa kutokupata huduma stahiki kutokana na ukosefu wa hela na pindi wakihoji juu ya huduma bure wanatakiwa kutoa vitambulisho vinavyowatambulisha kutoka halmashauri.

"Ni sawa na kusema kuwa huduma hii haipo kabisa kwa sababu halmashauri hazitoi vitambulisho na tukienda kupatiwa matibabu hakuna kinachoendelea tunaishia kurudi nyumbani bila kuhudumiwa, tunaomba serikali iingilie suala hili," alisema Lubadili Shirungu (84).

Aidha, Nipashe ilimtafuta Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Dk. David Mndeba, kujua juu ya utaratibu wa utolewaji wa huduma hiyo ya bure kwa wazee ambaye alieleza kuwa tatizo hilo lipo kwenye halmashauri ambayo inatakiwa kutoa vitambulisho kwa wazee hao ili wapatiwe huduma.

"Kwa sasa wazee wanatambulishwa kwa vitambulisho vya mpiga kura ambavyo siyo sehemu yake, hivyo halmashauri inaendelea kufuatilia namna ya kulitatua,"alisema Dk.Mndeba.

Kero hiyo iliibuliwa hivi karibuni katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Buchosa ambako Diwani wa Kata ya Nyakasasa, Deogratiasi Ivori, aliuliza lini halmashauri itaandaa vitambulisho vya matibabu kwa ajili ya wazee walio zaidi ya miaka 60 na kuendelea ili waweze kutibiwa bure.



Waandishi wa habari wa mkoa wa Shinyanga, wakiwa kwenye Bandari ya Kaskazini, jijini Mwanza juzi, walipokuwa katika ziara ya kujifunza namna uwekezaji wa bandari unavyochochea ukuaji wa uchumi nchini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bil.60/- kukarabati Bandari tatu Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** MWANZA


MENEJA Bandari Ziwa Victoria, Fredinand Nyathi, amesema serikali imetenga Sh.bilioni 60 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa bandari tatu ya Mwanza Kaskazini, Kemondo na Bukoba lengo likiwa ni kuboresha huduma. Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kutoka mkoani Shinyanga walipotembelea Bandari ya Mwanza Kaskazini kwa ajili ya kujifunza juu ya uwekezaji wa Bandari nchini.

Alisema serikali kwa sasa imekuwa ikizifanyia maboresho makubwa Bandari zake ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi pamoja na kupokea mizigo mingi, meli nyingi hali ambayo itachangia ongezeko la mapato na kukua kiuchumi.

"Katika Bandari hii ya Mwanza Kaskazini Serikali imetenga Sh.bilioni 18.6 kwa ajili ya kuboresha miundombinu yake na katika bandari zote tatu ikiwamo ya Kemondo na Bukoba zipo katika maboresho makubwa na mkandarasi yupo eneo la mradi na kitatumika kiasi cha Sh.bilioni 60 kuzikarabati," alisema Nyathi.

Alizitaja nchi ambazo zimekuwa zikihudumiwa na Bandari hizo tatu kwa kusafirisha mizigo kuwa ni Uganda, Rwanda, Burundi, pamoja na Kenya na kubainisha kuwa uboreshaji wa Bandari hizo utachukua muda wa miezi 18. Naye Ofisa Bandari ya Nchi Kavu ya Isaka, Abel Mshana, alizitaja nchi ambazo wamekuwa wakizihudumia katika usafirishaji wa mizigo kuwa ni Rwanda, Burundi, Uganda, Sudani Kusini na DRC, na kwamba Bandari hiyo ipo kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Bandari hapa nchini.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga, Greyson Kakuru, alisema katika ziara hiyo wamejifunza mambo mengi juu ya uwekezaji wa Bandari na namna zinavyofanya kazi katika ukuzaji wa uchumi wa nchi.




Baada ya mkanyagano wa Dipiwelidi sasa ni MTEKU!




## Waziri Ulega: Iinakuja na neema kwa wafugaji, wavuvi, wazalishaji nyama


# BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 1, 2023

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe


KONGAMANO KIMATAIFA LA CHAKULA AFRIKA

# Dk. Samia alivyoanza safari mapema, kilimo nchini chasonga bajeti 330%

**Na Peter Orwa**

KUANZIA Jumanne hadi Alhamisi wiki ijayo, katika Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, kunatarajiwa kufanyika Kongamano la 13 la Mifumo ya Chakula Afrika la kila Mwaka (AGRF).

Ni tukio la nchini lenye uhusiano wa moja kwa moja na tija kutoka utendaji wa mkuu wa nchi mwenyeji, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwamba amekubalika kutoka kwa umma huo wa bara alikotoka.

Dk. Samia anasema Tanzania imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa kongamano baada ya kufanikiwa katika shindano la kuandaa tukio hilo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, awali akatoa ufafanuzi kwamba zaidi ya washiriki 3,000 walitarajiwa kuwapo katika kongamano hilo, wakiwamo wadau wa sekta ya kilimo duniani, wawekezaji wa maendeleo, taasisi za fedha, watafiti wafanyabiashara wa kilimo, wakulima wakubwa na viongozi wa kiserikali.

Hata hivyo, wiki hii serikali imetoa ufafanuzi mpya kwamba imeshavuka malengo ya awali kwa kusajili washiriki 3200, huku matarajio mpya ni kufika washiriki 4,000 hadi pale mkutano utakaponza siku nne zijazo.

Mnamo Desemba mwaka jana, taarifa ya Ikulu kutoka mkutanoni nchini Marekani



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika moja ya ziara zake mashambani kwa wakulima. **PICHA: MTANDAO.**

alikokuwa Rais Dk. Samia, ikafafanua kwamba: "Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa kilimo...."

Chanzo cha uamuzi huo ulitangazwa na Waziri Mkuu mstaafu wa Ethiopia, Hailemariam Desalegn katika Jukwaa la Mtandao wa Chakula Afrika (AGRF), walikokuwa wote na Rais Dk. Samia, mkutanoni nchini Marekani.

Dk. Samia anaeleza imani yake namna mkutano utakavyoendelea kuimarishwa kwa mifumo ya chakula na kilimo katika vipaumbele vya serikali, kupeana taarifa na kutumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya mifumo imara ya chakula.

Ni matarajio yanayojikita katika namna maudhui husika yatajumuisha mjadala wa biashara miongoni mwa miji mbalimbali, ili kuchangia usalama wa chakula, ukuaji na ustahimili wake.

Ikirejewa ufafanuzi wa Rais kuhusu malengo ya mkutano, sasa ni kuzishawishi nchi zote za Afrika katika ajira kwa vijana, kila nchi barani Afrika kuweka wazi mikakati yake ya kuzifanikisha.

Taarifa ya Ikulu inatamka kwamba, Rais Dk. Samia katika uongozi wa nchi ameongeza zaidi ya mara tatu ya bajeti kutoka Dola za Marekani milioni 126.7 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, hadi kufika milioni 411.2 kwa mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 324 wakati huo.

Katika mwaka wa fedha uliopita, 2022/23, sekta ya kilimo ilikuwa na bajeti ya Sh. trilioni 41.5; sasa katika bajeti ya 2023/24 imepanda kuwa Sh. Trilioni 44.39, ambayo ni nyongeza ya Sh. Trilioni 2.89.

Waziri wa Kilimo anasema mnamo Machi mwaka huu kwenye uzinduzi rasmi wa usajili wa washiriki wa Kongamano la Usalama wa Chakula, akatamka wanaangazia zaidi kutumia mbinu bunifu zinazohakikishia dunia usalama wa chakula.

Katika hotuba yake kabla ya kuzindua usajili huo wa kongamano, Waziri Bashe akawaalika wadau wa kilimo wakiwamo na wataalamu wa mifumo ya chakula duniani.

Pia, akasisitizia umuhimu na nafasi ya viongozi wa Afrika kuwezesha usalama wa chakula ngazi za taifa na barani Afrika, kwa upekee nafasi ya vijana na wanawake.

"Wakati tukiendelea na jitihada za kuliwezesha Bara la Afrika kuwa kitovu cha usalama wa chakula duniani, tunapaswa kuwapa kipaumbele vijana na wanawake katika harakati hizi," anatamka Bashe.

**KINACHOFANYIKA NCHINI**

Mikakati inayoendeshwa na serikali ya awamu ya nne hivi sasa ni msingi na manufaa ya kutumika sekta kilimo nchini, inaangazia kwenye maeneo manne makuu: Chakula; biashara kwa bidhaa za ziada; malighafi ya uzalishaji; na ajira kwa umma.

Katika ngazi hiyo ya kimataifa, Dk. Samia akataja matarajio yake yanaangukia katika kujadili na kuimarisha mifumo ya chakula, pia kupeana taarifa baina ya

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

KONGAMANO KIMATAIFA LA CHAKULA AFRIKA

# Nafasi pekee kuwavuta wawekezaji kilimo, Rais abuni nchi kuwa kitovu mbolea Afrika

## • Dalili za kulisha bara yaanza kujionyesha

**Na Alpha Nuhu**

ZIKIBAKI siku nne hadi sasa,Tanzania imebeba matumaini makubwa kwa Mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika utakaoanza kwa siku tatu wiki ijayo, utakuwa na tafsiri chanya na pana kwa uchumi wa nchi na wadau wake kimataifa, katika sekta ya kilimo.

Ishara ya awali inatajwa kwamba ni neema na kichocheo cha kuwavuta wawekezaji wakubwa katika sekta ya kilimo nchini, wakitoka sehemu mbalimbali duniani.

Kimsingi, ni mkutano utakaojadili kwa kina mikakati ya kivitendo na njia sahihi za kulifanya bara la Afrika lijitegemee kwa usalama wa chakula, wadau wake ni

kutika makundi ya wataalam, watafiti, watunga sera,wanasiasa na wakulima wadogo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Kilimo iliyotolewa na Katibu Mkuu,Gerald Mweli,baadhi ya Marais wa Afrika wameshaonyesha nia ya kushiriki, wakimuunga mkono mwenyeji wao, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Baadhi ya wazungumzaji wakuu watarajiwa ni wakuu; Rais Dk. Samia, Waziri Mkuu wa zamani wa Ethiopia Hailemariam Dessalegn, Waziri wa Kilimo wa Tanzania, Hussein Bashe na viongozi wengine mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi.

Mkutano huo wa Dar es Salaam, unajikita zaidi katika azma kulikwamua bara Afrika, dhidi ya janga la njaa, ambalo wataalam wanaonya huenda likaikumba dunia kwa miaka ya usoni.

Viongozi wa Tanzania akiwamo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wanauona mkutano wa Dar es Salaam kama fursa ya pekee kwa Tanzania, taifa tajiri kwa rasilimali kuivuta dunia kujionea yaliyotendeka na yatakayotendeka, katika kuigeuza Afrika kuwa ghala la dunia kwa usalama wa chakula.

"Ni nafasi pekee ya kuimarisha uhusiano na ubia utakaosukuma mipango yetu ya kubadili mifumo yetu ya chakula," anaeleza Waziri wa Kilimo , Hussein Bashe na kuendelea:

"Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu, ambao mchango wake kwa pato la taifa ni sawa na theluthi moja, kama ilivyo katika nchi nyingi za Afrika.

"Jukwaa la Mifumo ya Chakula 2023 linalotarajiwa kuzua mijadala mizito kuhusu masuala ya fedha duniani, hasa katika kukidhi changamoto zinazolikabili bara la Afrika linapokuja suala la usalama wa chakula, yatajadiliwa kwa kina."

**KUTOKA TFRA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stephan Ngailo, anaipongeza serikali kuandaa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika 2023, kwamba utaifanya nchi itambulike kote duniani.

Anafafanua kwamba, kwa washiriki watakaokuwa mara yao ya kwanza kukanyaga ardhi ya taifa, lililojaliwa kwa rasilimali za kila aina, Dk. Ngailo, akieleza kwamba:

"Wanaotarajiwa kuhudhuria mkutano watabeba ulimwengu kuuleta Tanzania na kuibeba Tanzania na kuipeleka ulimwenguni. Jukwaa litakuwa fursa kwa Tanzania kujitwalia soko la chakula kinachozalishwa nchini mwetu.

"Mkutano huu una manufaa kwa nchi yetu, kwa sababu Tanzania ina mchango mkubwa kuhusu upatikanaji wa mbolea ambayo ni pembejeo muhimu kwa uzalishaji wa chakula. Kwetu sisi TFRA itakuwa fursa ya kueneza injili ya umuhimu wa mbolea katika kukuza uzalishaji katika kilimo."

Mchumi Mwandamizi wa TFRA, Elizabeth Bole, ambaye pia ni Kaimu Meneja wa Ununuzi Mbolea, huku akiahidi umakini katika kufuatilia kinachojiri mkutanoni, ana ufafanuzi:

"Mchango wa mbolea katika kilimo ni suala ambalo halihitaji mjadala mrefu, kwa kuwa uchumi wa Tanzana na nchi nyingine za Afrika unategemea sana kilimo. Ili uchumi ukue kwa kasi. ni lazima kuwapo matumizi sahihi ya mbolea."

Katika harakati za kuimarisha kilimo, serikali nchini mwaka jana, ilitenga shilingi bilioni 150 kama ruzuku ya mbolea kwa wakulima, ili kuwasaidia waongeze uzalishaji na kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo katika soko la dunia, hasa baada ya kuzuka kwa vita kati ya mataifa Russia na Ukraine.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakikagua mbolea ya kupandia, wakati alipotembelea kiwanda kipya cha mbolea jijini Dodoma, Desemba mwaka jana. **PICHA: MAKTABA.**

Kwa mujibu wa Dk. Ngailo, katika siku za usoni Tanzania itakuwa kitovu cha mbolea barani Afrika, kama mikakati ya sasa iliyobuniwa na serikali ya kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya mbolea, itakwenda kama ilivyopangwa.

Hadi sasa, Tanzania inashuhudia kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea ili kukidhi mahitaji makubwa ya bidhaa hiyo katika sekta ya kilimo.

Nia ya kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea, ni kuwapunguzia wakulima bei, ili mbolea ipatikane kwa urahisi kwa kuwafikia wakulima mahali waliko.

Lengo la kuwavuta wawekezaji katika ujenzi wa viwanda ni kuwa na soko linaloaminika la bidhaa hiyo kwa nchi jirani za Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika, pamoja na mataifa mengine ya Ulaya, ambayo yamekuwa yakiagiza mbolea kutoka kiwanda cha Minjingu mkoani Manyara.

Anataja mahitaiji hayo kwa wakulima wa Tanzania katika miaka ya karibuni, yameongezeka kutoka tani 42,000 mpaka tani165,000,baada ya kuwapo jitihada za kuwaelimisha wakulima kutumia mbolea, ili waongeze tija katika mashamba yao.

Katika hilo, Mkurugenzi wa TFRA Dk.Ngailo anataja furaha yake kwamba ongezeko la matumizi ya mbolea nchini limezaa matunda, baada ya kushuhudia ongezekola uzalishaji chakula nchini kutoka tani milioni 17 hadi tani milioni 20.

"Kazi ya kuwaelimisha wakulima kutumia mbolea ni suala endelevu, kwa kushirikiana na serikali za mitaa. Kuna uwezekano mkubwa kwa wakulima wengi Tanzania kutumia mbolea na hatimaye kulilisha bara la Afrika," anaeleza Dk. Ngailo.

"Ruzuku ya mbolea imesaidia sana wakulima kununua mbolea kwa wingi ikilinganishwa na miaka ya nyuma" ananena Dk.Ngailo, kwamba ongezeko la matumizi yake miongoni mwa wakulima,limewapa viongozi ari kujiamini kwamba, Tanzania katika miaka michache ijayo itafikia lengo lake kulisha bara Afrika kutokana na ziada ya chakula inayozalishwa.

Hapo anaungwa mkono na Mchumi Mwandamizi wa TFRA, Elizabeth Bole, akifafanua dhamira yaTanzania kujitosheleza kwa chakula, ikiwa ni ghala la kuaminika barani Afrika na dunia.

Mchumi Elizabeth, anasema mkutano ujao nchini wa Jukwaa la Chakula Afrika 2023, utakuwa na mengi ya kujionea, yatakayofaa kuigwa na mataifa mengine barani Afrika.

Watalamu hao, wasimamizi wa hazina ya mbolea kitaifa, wanataja matarajio makubwa ya mkutano huo, katika mtazamo wake, Mkurugenzi wa

TFRA, Dk. Ngailo, kwamba dunia itakuja kushuhudia yaliyopo na itaondoka na mafunzo kwenda kuyapandikiza sehemu nyingine na hivyo kuliuza jina la Tanzania ughaibuni.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz

OFISI YA ...
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE
CHAMWINO
S.L.P ...
40400 DODOMA

Washington, DC
13 Desemba, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TANZANIA KUWA MWENYEJI WA JUKWAA LA MTANDAO WA CHAKULA AFRIKA (AGRF) 2023

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameridhi[...] Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano mkubwa wa Kilimo utakaohusisha Viongoz[...] watu mashuhuri na wadau wapya 3,000.

Uamuzi huo umetangazwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia, Mheshimiw[...] Hailemariam Dessalegn katika Jukwaa la Mtandao wa Chakula Afrika (AGRF) nchi[...] Marekani.

Rais Samia amesema anatarajia mkutano huo utaendeleza uimarishaji wa mifumo y[...] chakula na kilimo katika vipaumbele vya Serikali, kupeana taarifa na kutumi[...] teknolojia ya kisasa kwa ajili ya mifumo imara ya chakula.

Pia Rais Samia amesema wadau mbalimbali watakaohudhuria wataweza kujadi[...] namna ya kuimarisha biashara miongoni mwa miji mbalimbali ili kuchangia usalam[...] wa chakula, ukuaji na urumilivu.

Mbali na hayo lengo lingine ni kushawishi nchi zote juu ya ajira kwa vijana ambap[...] kila nchi barani Afrika itaweka wazi mikakati yake ya malengo ya ajira hizo na namn[...] ya kufanikisha.

Katika kuimarisha shughuli za kilimo serikali ya Tanzania imeongeza bajeti yak[...] karibu mara nne katika sekta hiyo kutoka dola za Kimarekani milioni 126.7 kw[...] mwaka 2021/2022 hadi dola milioni 411.2 mwaka 2022/2023.

Rais Samia amewasili nchini Marekani kuhudhuria mkutano wa siku tatu wa Waku[...] wa Nchi wa Afrika na Marekani utakaohusu masuala mbalimbali ya kimaendele[...] pamoja na mikutano mengine ya kimkakati.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

# Dk. Samia alivyoanza safari mapema, kilimo nchini chasonga bajeti 330%

**INATOKA UK.11**

nchi, maboresho kiufundi kwa ajili ya mfumo wa chakula.

Vilevile, Rais akautaja ni ulingo muhimu wa wadau mbalimbali kuijadili biashara kati yao, ikiwamo katika suala la ushirikiano kati ya miji, kuchangia usalama na ukuaji katika uzalishaji chakula kimataifa.

Kuna mambo kadhaa yanatajwa sasa kwa Rais Dk. Samia anayoyaorodhesha katika utekelezaji, ikijumuisha kuimarisha utafiti; kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano, pia miche ya zao la michikichi; kuimarisha upatikanaji pembejeo za kilimo; kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo; hali kadhalika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kujengea miundombinu.

**DIRA YA WIZARA**

Kwa mujibu wa Waziri Bashe, wakulima nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi ya kilimo, hadi sasa kumekuwapo mchango mkubwa katika kuhakikisha nchi inakuwa na usalama, hata mauzo yake nje ya nchi kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 994.5 mwaka 2021 hadi dola Bilioni 1.38, kufikia Aprili mwaka huu.

Anarajea idadi ya Watanzania milioni 61.74 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka huu, kati yao asilimia 65.6 sawa na zaidi ya Watanzania milioni 40, maisha yao ya kila siku yanategemea moja kwa moja sekta kilimo.

Vilevile, uchambuzi huo wa Waziri Bashe, kupitia makakadirio ya kibajeti bungeni mwaka huu, kuna jumla ya kaya 11,659,589 ya Watanzania chini ya uongozi wa sasa wa Rais Dk. Samia, kati yao 5,088,135

zinategemea moja kwa moja kilimo. Hao ni sawa na asilimia 43.6 ya kaya zote nchini.

Vilevile, anataja kitaifa sekta ya Kilimo imeendelea kukua vizuri katika miaka kadha iliyopita, huku sasa ikichangia asilimia 26.1 ya Pato la Taifa.

Vilevile anaitaja kutoa ajira kwa wananchi wastani wa asilimia 65.6; ilhali inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda na asilimia 100 ya chakula nchini.

Pia, Waziri Bashe anaitaja sekta Kilimo katika awamu ya sita, anataja kuwa na mkakati wa kukabiliana na upungufu wa chakula nchini, serikali ikiendelea kuongeza uwezo wake kuhifadhi chakula kutoka tani 251,000 za sasa hadi 506,000.

Lingine ni serikali ya awamu ya sita, imeanza upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya uhifadhi itakayoongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kufikia tani milioni tatu ifikapo mwaka 2030.

Waziri anataja lengo lililopo ni kuhakikisha taifa linakuwa na uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutumia miezi sita pindi inapotokea janga, ukiwa ni mkakati wa kulinda uchumi na heshima ya nchi.

Hadi sasa, serikali tayari iko katika mpango wa taifa kujenga maghala ya kuhifadhi nafaka kila mkoa, mkakati uliotangazwa kwa wakati tofauti na Rais Dk. Samia, pia kusisitizwa

na Waziri wa Kilimo, Bashe, hatia ionayoenadna kudhibiti uuzaji holela wa vyakula nje ya nchi, ili uwapo katika utaratibu unaoinufaisha nchi na wakulima wake.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Baada ya mkanyagano wa Dipiwelidi sasa ni MTEKU!




**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

MMEJIKALIA nyumbani kama familia, hamna hili wala lile, bali mnajadiliana jinsi mambo yanavyoendelea duniani, huku mkilinganisha na maisha yalivyo magumu, mara anaingia mkuu wa familia amejawa bashasha.

Kama ada mnanyamaza na anakaa na kusalimiana kwa heshima zote na kumsikiliza kaja na nini jioni hii. Anajikoholesha kidogo na ghafla anakwambieni pamoja na umri mlionao, mnatakiwa kujifunza kunyonya maziwa kwa mama yenu.

Bila shaka mnapatwa na mshituko na taharuki na kuzubaa kidogo, kabla ya kutulia, mmoja wenu hususan anayekuzidini umri anamwuliza baba yenu anamaanisha nini kukwambieni hivyo, huku akijua mlishakoma kunyonya si leo.

Huku mkiwa bado mnamshangaa kwa kauli ile, anafumbua kinywa na kukusisitizeni, lazima mjifunze tena na kama hamtaki nyumba hiyo hakutanyweka maziwa tena, mpaka mtakapokubali kujifunza upya kunyonya kwa mama yenu.

Lazima, baadhi yenu mnaomjua baba yenu ambaye hanywi pombe wala kuvuta sigara hata bangi, mnatulia na kumtazama huku naye akikushangaeni kwa nini mnamtazama vile na anasisitiza kwamba anafanya hivyo kwa manufaa na maslahi yenu mapana.

Nyote mnaamini kwamba, lazima kuna jambo yawezekana mzee kapatwa na mashetani au pepo wabaya huko njiani mpaka kuja na maagizo ya kushangaza kama hayo, ya watu wazima kama nyie, kurudia matiti ya mama eti kunyonya maziwa, jambo ambalo mlishalifanya mkaacha. Mnakataa kwa kumwambia haeleweki.

Hebu oneni hapa. Juzi kati hapa, akiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Daktari Damas Ndumbaro akatutangazia kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania hawaijui Katiba iliyopo sasa ya mwaka 1977, kwamba kutokana na udhaifu huo, si rahisi kuja na Katiba sasa.

Kasema kinachotakiwa ili kuja na Katiba nzuri, ni kuandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Katiba kwa Umma (MTEKU 2023-2026) ili wananchi warudi madarasani kujifunza Katiba na wakishaielewa barabara, ndipo mchakato uanze!

Daktari anakuja na kauli hiyo akijua fika kuwa mwaka 2012 kulikuwa na masuala hayo hayo ya Katiba, watu walizinguka nchi nzima kutafuta maoni ya wananchi, wakayatoa na kukusanywa na kuchakatwa.

Tunakumbuka mchakato ule chini ya Jaji Joseph Warioba na Bunge Maalumu chini ya Samweli Sitta na Samia Suluhu Hassan ulikwenda vizuri, lakini bahati mbaya kikatokea cha kutokea, tukaishia tulikoishia.

Leo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge hilo, Samia, anasema tuanze mchakato ya kitaaluma ya daktari, hiyo inafaa mpaka baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2025, tuache kwanza MTEKU ufanye kazi yake.

Najaribu kuikumbuka kidogo timu ya kitaalamu, zama za mchakato uliopita; chini ya Jaji Joseph Warioba, Jaji Augustino Ramadhani, Samwel Sitta, Samia, Profesa Mwesiga Baregu, Riziki Mngwali, Daktari Sengondo Mvungi, Richard Lyimo, John Nkolo, Alhaji Said El-Maamry, Jesca Mkuchu na Profesa Palamagamba Kabudi.

Humphrey Polepole, Yahya Msulwa, Esther Mkwizu, Maria Kashonda, Al-Shaymaa Kwegyir, Mwantumu Malale, Joseph Butiku, Daktari Salim Ahmed Salim, Fatma Said Ali, Omar Sheha Mussa, Raya Suleiman Hamad, Awadh Ali Said, Ussi Khamis Haji, Salma Maoulid, Nassor Khamis Mohammed, Simai Mohamed Said na Muhammad Yusuf Mshamba.

Pia, Kibibi Mwinyi Hassan, Suleiman Omar Ali, Salama Kombo Ahmed, Abubakar Mohamed Ali na Ally Abdallah Ally Saleh waliokuwa katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mpya, ni wenye ufahamu wa kutosha katika kuunda katiba wakati huo mwaka 2012.

Naweza kujiuliza kuwa hivi mpaka tupate Katiba mpya lazima kila Mtanzania aijue yote, kila kipengele na kila mstari, ndipo tuibadilishe kweli?

Nadhani si kila jambo liamuliwe na asilimia 100 ya Watanzania na ndiyo sababu hata nchi kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, hatukuhitaji asilimia 100 bali asilimia 20 tu ilitosha.

Nahofu tusije kuzaa malumbano mengine mapya, hata kabla ya haya ya Dipiwelidi hayajaisha. Ni maoni yangu, tukiegemea sana elimu kwanza, basi tutazidi kutanua ufa uliojitokeza kwenye la 'nkataba' wa uwekezaji bandarini. Ninadhani mchakato wa Katiba uanze sasa. Alamsiki!

BIASHARA

KONGAMANO KIMATAIFA LA CHAKULA AFRIKA

# Waziri Ulega: Linakuja na neema kwa wafugaji, wavuvi, wazalishaji nyama

## • Kicheko kwa mama na kijana, nacho kipo

**Na Maulid Mmbaga**

KUELEKEA Mkutano wa AGRF, Nipashe imezungumza na mshiriki Mkurugenzi wa kampuni ya Ufugaji na Maendeleo ya Vijana na Wanawake Vijijini (AKM) Elizabeth Swai, kuhusu mkutano huo, akisema AGRF itakuwa na uwezeshaji mwingi ikiwemo kujifunza kuhusu masuala ya ufugaji.

Anaeleza kuwa suala la kujifunza ni muhimu na kwamba kutakuwa na mashirika makubwa ambayo yatakuja na teknolojia tofauti ambazo ni muhimu kwa Watanzania kujifunza.

Aidha, anasema AGRF wanaitazama kama miongoni mwa fursa kubwa na neema uliyokuja katika sekta ya ufugaji, kwa kuwa kutakuwa na watu wengi wenye nia na mitaji watakaotaka kuja kuwekeza, akieleza kwamba katika ufugaji wanahitaji uwekezaji mkubwa kwa sababu katika sekta hiyo kuna mnyororo mingi ya thamani.

"Ufugaji unagharama, mfano mimi ninalea vifaranga 15,000 katika kuwalea hadi wawe kuku wakubwa watage inagharimu fedha nyingi kwahiyo ni uwekezaji mkubwa ambao inabidi tutumie hii fursa ya AGRF kuangalia kwamba sisi tutanufaika na nini.

"Inatakiwa tujue tutanufaikaje kutoka kwenye elimu, uwekezaji, ushirikishanaji wa kibiashara, kutafuta mikopo, taarifa na kuongeza uelewa, nafikiri ni muhimu kwa Watanzania kuhudhuria mkutano huo," amesema Elizabeth.

"Tanzania tunaweza kulisha dunia, tuna nafasi kubwa na vijana wengi ambao wananguvu lakini hawawezeshwi kujua ni shughuli gani za kuwaingizia kipato ambazo wanaweza kufanya, kwa hiyo kutokana na AGRF, tunaweza kupata fedha na ushirikiano wa kibiashara tukaweza kuwawezesha vijana zaidi," amesisitiza Elizabeth.

### UMUHIMU WA AGRF

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, anasema mkutano huo kwa upande wa wizara wanauchukulia kama kielelezo na fursa kubwa kwa wadau wa uvuvi, wazalishaji wa nyama, samaki, pia wanaojihusisha na ng'ozi, mayai, kuku na wanyama wengine.

Anasema AGRF ni wakati muafaka ambao utawaleta pamoja



Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega, katika moja ya ziara zake kikazi, akijumuika na wafugaji. **PICHA: MTANDAO.**

wafugaji wa wanyama na samaki, wavuvi, wawekezaji, taasisi za kifedha na wanaotaka kufanya biashara ya majani.

"AGRF ni mahali tutakapopata uzoefu wa uzalishaji, teknolojia, mitaji ya kufanyia biashara, pamoja na masoko ya biashara zetu, wadau wote ninawakaribisha kushiriki kikamilifu katika siku hizi nne za mkutano kwani hii ni fursa adimu.

"Sisi Tanzania imekuwa ni wakati mzuri kwetu, tuitumie kufungua fursa za uwekezaji katika nchi yetu, tunahitaji teknolojia za kisasa kwenye uzalishaji, katika mifugo, uvuvi na kilimo, tunataka tuilishe dunia wakiwemo majirani zetu, na ili tufanye hivyo ni lazima tuzalishe vya kutosha," anasema Waziri Ulega.

### NAFASI YA VIJANA

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao katika Wizara ya Kilimo, Nyasabwa Chimagu, anatoa wito kwa vijana na wanawake kujitokeza kwa wingi mkutanoni, ili kupata fursa ya kujitangaza, kupata masoko na kujifunza ujuzi mbalimbali kutoka mataifa mengine.

Anasema, kuna fursa nyingi zitakazopatikana wakati wa mkutano, hata baada ya hapo, ikiwaemo uwekezaji na masoko, na kwamba kutokana na mageuzi ya mifumo ya chakula serikali imetenga Shilingi milioni 800 kusaidia vijana na wanawake kijiendeleza katika kilimo.

"Serikali imetenga pesa hizo kwaajili ya vijana kwani wao wataweza kujiajiri lakini pia kutengeneza ajira kwa wenzao, pia suala hilo tunaamini litakuza mnyororo wa thamani katika sekta hii kwa ujumla," anasema Chimagu.

Aidha, anabainisha kuwa fursa zingine zitakazopatikana AGRF ni kusainiwa kwa mikataba ya makubaliano (MoU), ili kukuza na kuendeleza miradi inayotokana na kilimo.

Anaeleza kuwa uwekezaji utakaojitokeza katika mkutano huo pia utakua fursa kwa wakulima wadogo, wakati na wakubwa kupata masoko na kukuza biashara zao.

"Tukizungumzia uwekezaji ni suala pana sana kutakuwa na uwekezaji kwenye kilimo, utalii, uzalishaji wa mbegu na usafirishaji, na matumizi makubwa ya teknolojia yanahitajika ili kuhakikisha mnyororo wa thamani unakuwa," anasema Chimagu

Vilevile anawataka vijana na wanawake wenye ubunifu wanapaswa kujitokeza kwa wingi ili waweze kujitangaza kimataifa.

### WADAU WA MAZIWA

Katika hatua nyingine Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) inatoa wito kwa wadau wanaojihusisha na tasnia ya maziwa kushiriki kikamilifu mkutano wa AGRF, huku ikieleza kwamba bidhaa hiyo ina umuhimu na mchango mkubwa kwa afya ya mlaji na katika kuongeza pato la taifa.

Mtaalamu wa maziwa wa TDB, Francesco Mussa, anasema pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji lakini bado kuna uhaba wa bidhaa hiyo nchini licha ya kwamba uhitaji ni mkubwa, na kwamba AGRF itatumika kutangaza fursa zinazotokana na maziwa hali itakayosaidia kuongeza uzalishaji.

Anasema mkutano huo utasaidia kuongeza kasi ya ushindani endelevu wa wadau kwa maendeleo endelevu ya tasnia ya maziwa. Na kwamba TDB inaendelea kufanya kazi na wadau mbalimbali ili kufikia malengo ya kuwa na tasnia inayokuwa na kuchangia uchumi wa nchi na watu wake, lishe, na ajira.

"Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 3.4 hadi 3.6 sawa na ongezeko la asilimia tano, hii ni kutokana na mabadiliko ya teknolojia na kufuata kanuni za ufugaji bora. Kati ya lita hizo zilizozalishwa, bilioni 2.4 zimetoka kwa ng'ombe wa asili na bilioni 1.2 wa maziwa.

"Licha ya uzalishaji kuongezeka, wastani kiuzalishaji uko chini hivyo TDB tunaendelea kutoa elimu ya ufugaji bora kwa lengo la kuwasaidia wafugaji kufuga kibiashara."

Vilevile, anasema mahitaji ni makubwa hivyo husababisha uingizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje na kwamba kwa mwaka 2022/23 lita milioni 11.6 zenye thamani ya bilion 22.7 ziliingizwa nchini.

Anabainisha kuwa katika kudhibiti uingizwaji holela wa maziwa na bidhaa zake, TDB inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Na kusimamia utoaji wa vibali vya kuyaingiza kwa kuzingatia mahitaji ya soko na kulinda viwanda vya ndani.



Mfugaji kuku anayefunzwa na kampuni ya Ufugaji na Maendeleo ya Vijana na Wanawake Vijijini mkoani Dar es Salaam, akijifunza kwa vitendo. **PICHA: MAULID MMBAGA**





Vijana waliohitimu mafunzo ya mradi wa kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo wa Jenga Kesho Bora (BBT), wakiwa katika eneo la kijiji cha Ndogowe, mkoani Dodoma juzi, kuangalia mashamba ya pamoja yanayogawiwa na serikali kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mazao mbalimbali baada ya kuhitimu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Serikali yatafuta wafadhili kuondoa magugu Ziwa Jipe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imeanza kutafuta wafadhili wa mradi wa hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni sita (Sh. bilioni 15) ili kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe.

Waziri wa Nchi wa Ofisi hiyo, Dk.Selemani Jafo alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mwanga (CCM), Joseph Tadayo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itatekeleza mradi wa kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe.

Akijibu swali hilo, Dk.Jafo alisema serikali imeona tatizo la uharibifu wa mazingira unaotokana na kuenea kwa magugu maji katika Ziwa Jipe.

"Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira tayari zimefanya tathimini ya uharibifu uliopo na kuandaa andiko la mradi wa hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji wenye thamani ya takribani Dola za Marekani milioni sita kwa ajili ya kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe ambapo hadi sasa jitihada za kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali zinaendelea,"alisema.

Alisema nia ya serikali ni kuhakikisha inarejesha ikolojia ya Ziwa Jipe ili kuleta manufaa kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo pamoja na uhifadhi wa mazingira. "Serikali inamhakikishia mbunge kwamba mara fedha zitakapopatikana itatekeleza mradi huu mara moja, " alisema.

Kadhalika, alisema andiko hilo ni kwa ajili ya Ziwa Jipe na Chala na kwamba ofisi hiyo itaangalia fursa zitakazokuwapo hata kwa kuwa na mradi wa muda mfupi.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedasto Manyinyi, alisema kwenye Ziwa Victoria mwaka jana lilichafuka na kusababisha samaki wengi kufa na walipotumwa wataalamu walisema chanzo ni kinyesi cha ng'ombe.

"Serikali ina mpango gani kuhakikisha hali hiyo haijitokezi tena ili wananchi wa Kanda ya Ziwa wasiendelee kupata hasara," alihoji. Dk.Jafo akijibu swali hilo alikiri kujitokeza kwa tatizo hilo kwenye Ziwa Victoria akisema lengo la serikali siyo wananchi kuendelea kupata hasara.

Alisema: "Kwenye maeneo mbalimbali tuliyoona tatizo ni uharibifu wa mazingira mbali na Ziwa Jipe hata Ziwa Babati kuna ongezeko la magugu maji ndio maana Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imejipanga kuandika maandiko mengi ili maeneo haya yawasaidie wananchi na kuinua uchumi wao," alisema.

# LRCT yaziita taasisi zenye vikwazo vya kisheria

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imeaziagiza taasisi mbalimbali nchini zenye vikwazo vya sheria wanazozitekeleza kupeleka maoni kwa tume hiyo ili kufanyiwa mapitio na utafiti wa kina.

Imesema hatua hiyo itasaidia kuepuka maboresho ya sheria kufanyika mara kwa mara.

Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Griffin Mwakapeje akizungumza juzi mjini hapa, alisema sheria nyingi zinazofanyiwa marekebisho bila kupitia tume hiyo na zimekuwa hazifanyiwa utafiti wa kina, hivyo kuruhusu mabadiliko ya mara kwa mara .

"Sheria inatungwa Januari ukifika Agosti sheria inahitaji mabadiliko, hii inakuwa si afya katika mfumo wa utungaji wa sheria, tunataka mtuletee maoni sisi tufanye utafiti wa kina ili sheria zetu zidumu kwa miaka mingi bila kurekebishwa kwani ni jukumu la tume kufanya mapitio na utafiti wa sheria zote za Tanzania," alisema. Mwakapeje alisema ni jukumu la tume kufanya mapitio na utafiti wa sheria zote za Tanzania ili ziwe na manufaa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Adha, alisema tume hiyo imeanza ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa utendaji kazi za mapitio, tathmini na utafiti wa sheria mbalimbali za Tanzania Bara ili kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za nyaraka.

Alisema mfumo huo utakaojulikana kwa jina la Law Reform Management Information System (LRMIS) utasaidia kurahisisha mtiririko wa utendaji kazi, kufanya tathmini mbalimbali zitakazosaidia kubaini idadi ya mapendekezo ya tume yaliyotumika katika maboresho au kunda sheria mpya.

Mwakapeje alisema kwa kutumia mfumo huo utasaidia kupunguza gharama na muda kwa kuwa utakuwa na uwezo wa kuwasiliana na mifumo mingine ya taasisi za kisheria ikiwemo mifumo ya Wizara ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na mifumo ya Mahakama.

Alisema Tanzania kuna sheria zaidi ya 450 ambazo wanapaswa kuzifanyia mapatio ili kuona zinaendana na uhalisia katika mazingira ya sasa, huku akibainisha kwamba kuna maeneo mengine mapya ambayo huibuka kila siku yanayohitaji kutengenezewa sheria.

# PPRA yahimiza makundi maalum kujisajili NeST

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imewasisitiza watu waliopo kwenye makundi maalum ambayo ni vijana, wazee, wanawake na watu wenye ulemavu kujisajili kwenye Mfumo Mpya wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao (NeST), ili kunufaika na fursa za ugawaji wa zabuni za umma nchini.

Akizungummza jana jijini hapa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi alisema kuwa Mfumo wa NeST unawatambua na kuwazingatia wazabuni waliopo kwenye makundi hayo.

"Mfumo unawatambua watu wa makundi maalumu, kwa hiyo wanachotakiwa kufanya ni kufuata taratibu za kurasimisha vikundi vyao katika ngazi za halmashauri kisha wajisajili kwenye mfumo wa NeST," alisema Maswi.

Aidha, alisema kuwa katika Mfumo wa TANePS usajili wa makundi maalumu haukuwa mkubwa, hivyo amewasihi wenye sifa za kuwa makundi maalum na wanahitaji kushiriki zabuni za umma kujisajili katika mfumo wa NeST ambao ni rafiki zaidi kwa watumiaji wote.

"Serikali yetu inawajali watu wote na inataka kila mtanzania mwenye sifa aweze kushiriki zabuni za umma na kujiinua kiuchumi, sio tu kwa kampuni kubwa au watu binafsi waliosajiliwa pamoja na watu ambao wako katika uchumi wa chini ambao wanaweza kushiriki kupitia fursa ya makundi maalum hata bila kuwa kampuni,"alisema.

Alisisitiza kuwa zipo kazi nyingi ambazo kwa mujibu wa sheria zimetengwa kwa ajili ya makundi maalumu na kwamba mfumo wa NeST utaongeza kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wazabuni kwa kuwa unaongeza uwazi, ushindani na kuondoa urasimu usio na sababu za msingi.

Kadhalika, alisema fursa za ugawaji wa zabuni kwa makundi maalumu zinasimamiwa na kushughuliwa kwa kuzingatia vifungu vya Sheria ya Ununuzi ya Umma sura 410 inayozitaka taasisi zote za umma nchini kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa mwaka kwa ajili ya makundi maalumu.

"Kwa mujibu wa mwongozo wa makundi maalumu uliotolewa na PPRA mwaka 2020, makundi maalumu yamepewa asilimia 10 kwa vijana, asilimia 10 kwa watu wenye ulemavu, asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa ajili ya wazee,"alisema.

Maswi alisema kuwa PPRA bado inaendelea kutoa mafunzo wezeshi ya matumizi ya mfumo wa NeST kwa wazabuni na taasisi nunuzi kote nchini ili kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania wanajengewa uwezo na kuchangamkia fursa katika ununuzi wa umma nchini.







Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuja na Kushoka Tools inayojihusisha na uzalishaji wa mashine za kutengenezea nishati mbadala, akitoa elimu ya utengenezaji wa mkaa kwa kutumia taka mbalimbali kwa vijana, wakati wa mafunzo yaliyofadhiliwa na Taasisi ya Tulia Trust, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Majambazi waua, wajeruhi mhasibu Ruvuma

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wanaodhaniwa kuwa ni majambazi wamemuua mkazi wa Madaka mkoani Ruvuma, Faraja Luoga (35) na kumjeruhi Golden Luoga (33) ambaye ni mhasibu wa Umoja wa Mawakala kwa kumpiga risasi.

Tukio hilo limetokea Agosti 29 saa tatu usiku nyumbani kwao Mtaa wa Kambarage eneo la Galuhenga wilayani hapa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe Dk. Winfred Kyambile alisema majira ya saa nne usiku walipokea watu wawili wanaume mmoja akiwa amefariki.

"Bahati mbaya mmoja tulimpokea akiwa ameshapoteza maisha, mmoja tulimuwahi tukampa huduma za haraka, yupo wodini anaendelea vizuri ingawa bado anaweweseka kwa sababu tukio lilikuwa la kutisha na huyo mwingine chanzo kilichomuua ni kuvuja kwa damu kwa sababu alipingwa risasi upande wa kushoto ikaingilia maeneo la tumboni, nafikiri mifupa ilikatika mule ndani kwa hiyo alitoka damu nyingi"alisema Kyambile.

Nipashe ilifika eneo la tukio na kuzungumza na majirani ambao walisema walisikia milio miwili ya risasi ikitokea nyumbani kwa jirani yao huyo.

"Majira ya saa tatu na kama dakika tano hivi tukasikia milio miwili ya risasi na baadae tukatoka na kukuta wakiwa wamelala chini huku wakiwa wamepigwa risasi, damu zikiwa zinawatoka mmoja alikuwa amepigwa kifuani na mwengine maeneo ya kwenye paja. Tuliwachukua na kuwapeleka Hospitali ya Rufaa" alisema jirani ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini.

Jirani huyo alisema marehemu alifika hapo kwa mdogo wake kupumzika wakitokea wilayani Ludewa msibani na ikifika ili asubuhi aendelee na safari yake ya kwenda nyumbani Madaba.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kambarage, France Msanga alisema alipigiwa simu majira ya saa 3: 20 usiku ndipo alipofika eneo la tukio.

Alisema: "Hadi majira ya saa mbili alionekana yupo na mwenzie chaugingi (katikati ya mji wa Njombe), inaonekana ni watu waliokuwa wanamfuatilia kwa sababu walikuwa watu wawili wenye siraha ainaya ya SMG, wakaingia mpaka sebuleni wakapiga risasi ukutani wakachukua begi wanaondoka sasa wakawa wanaangalia wanaenda wapi wakawapiga risasi mlangoni"

Aliongeza: "Hili ni tukio la pili jingine lilikuwa mwezi wa nane kuna mtu aliporwa fedha kama Shilingi milioni 10 alifuatwa nyumbani lakini hawakumdhuru kwa hiyo yanazoeleka".

Grace Mgeni alisema matukio hayo yamekuwa ni ya kujirudia kila wakati kwa sababu wapo mawakala wengine ambao wamefanyiwa matukio ya namna hiyo.

"Huyu kama sio wakala wa tano basi wa saba, kuna wengine wanagongwa nondo wengine wanapingwa bisibisi lakini hatuoni chochote ndio mpaka hili tukio limetokea linatusikitisha, linatuumiza wana Njombe.

Mawakala tunaisha tunaomba vyombo vya usalama vitusaidie haya mambo yatokomezwe Njombe tunakufa, tunaisha juzi kuna mtu amechomwa bisibisi juzi kuna mtu amepigwa nondo kwa hiyo mawakala wanavamiwa wanafanya kazi katika mabaya, tunauchungu" alisema Mgeni.

"Ni mbaya sana kwa sababu mawakala tunawindwa sana mpaka majumbani kwa kweli hata hamu ya kazi tunaona haipo tena tunatoa huduma iliyo nzuri lakini watu wanaroho mbaya hawapendi tufanye kazi, mimi binafsi inaniuma sana, mawakala tunavamiwa kila kukicha, wengine wapo Hospitali ya Kibena wamekatwa mikono" alisema Telesia Mgina.

Makamu Mwenyekiti wa Mawakala Mkoa wa Njombe, Rehema Mabuga alisema tukio hilo sio la kwanza kutokea ni tukio la sita.

"Matukio haya yanatokea muda ambao ni rafiki, tunafunga mapema saa 12 lakini wakati huo huo matukio yanaendelea kutokea, inatushtua sana kwa sababu kwa muda huo matukio yanapokea maana yake doria bado huwa zinapita ni mapema sana, matukio yamekuwa mengi kwa wakati mmoja"alisema.

Hata hivyo aliliomba Jeshi la Polisi kuchukua hatua kwa sababu jambo hilo sio geni kwa sababu limeshasababisha hasara na vifo kwa watu.

"Kwa haya yanayoendelea tunafikiria tusitishe hii huduma kwa muda au uhai wetu au tufunge mapema, tufunge hata saa 10 kama wanavyofunga mabenki kwa sababu tunajua hii ni huduma muhimu kwa jamii inayotuzunguuka lakini kwa njia hii inayoendelea Njombe labda tusitishe kufunga mapema huduma zetu au mpaka tupate hatma ya upande wa pili"alisema Mwenyekiti wa Mawakala Mkoa wa Njombe, Erasto Mbembati.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, John Imori, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo huku akisema jitihada za kuwatafuta wahalifu zinaendelea.

# Wakulima wa chai walia ukosefu vitendea kazi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKULIMA wadogo wa chai katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamesema wanashindwa kuvuna vizuri majani ya chai kutokana na kutokuwa na zana za kisasa zikiwemo mashine na mikasi ya kisasa.

Waliyasema hayo juzi wakati wa kukamilisha mafunzo ya mwaka mmoja ya kilimo cha kisasa cha zao hilo, yaliyofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) ambayo yalivihusisha vyama vya wakulima (AMCOS).

Mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa na shirika lisilokuwa la kiserikali la IDH ambapo wakulima walioshiriki walikuwa 797 na yalikuwa yanafanyika kupitia mashamba darasa ya zao hilo yaliyoandaliwa kitaalamu.

Mmoja wa wakulima hao, Mariam Mwakanyamale alisema wakulima wengi wamekuwa wakichuma majani ya chai kwa kutumia mikono jambo ambalo linapunguza ufanisi hasa kwa wale wanaomiliki mashamba makubwa.

Alisema ukosefu wa vifaa hivyo kunasababisha wakati mwingine washindwe hata kuhudumia mashamba yao na hivyo akawaomba wafadhili mbalimbali kuwasaidia vifaa ili waongeze tija kwenye uzalishaji wa zao hilo.

Alisema kwa sasa soko la majani ya chai lipo na wakulima hawalazimiki kusafirisha kwenda kuuza mbali lakini kikwazo kinakuwa kwenye uvunaji wa majani.

"Tunaamini kwamba serikali inazitambua kero zetu lakini wakati mwingine inaweza isiwe na uwezo wa kuzitatua kwa haraka, tunawaomba wadau mbalimbali watusaidie kama ambavyo hawa wenzetu wa IDH wametusaidia mafunzo," alisema Mariam.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ally Said alisema Serikali italifanyia kazi suala la upatikanaji wa vifaa hivyo kwa wakulima ili wakuongeza tija kwenye uzalishaji pamoja na kukuza mapato yatokanayo na zao hilo.

Alisema watawasilisha ombi maalumu katika Wizara ya Kilimo ili wasaidiwe namna ya kulitatua huku akisisitiza kuwa wilaya hiyo ni miongoni mwa wilaya zinazozalisha kwa wingi zao hilo.

Alisema sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza kuipatia halmashauri hiyo mapato na hivyo akasisitiza kuwa inatakiwa kuboreshwa ili iwe na tija zaidi.

## Vijana 300 wajengewa uwezo kutengeneza nishati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya vijana 300 kutoka kata 36 za Jiji la Mbeya wamejengewa uwezo wa kutengeneza nishati mbadala kwa kutumia mabaki ya mazao na miti ya mbao ili kujiongezea kipato na kulifanya jiji hilo kuwa safi.

Nishati hiyo inatajwa kuwa itakuwa inatumiwa na taasisi mbalimbali zenye idadi kubwa ya watu zikiwemo shule, vyuo, magereza na majeshi ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuja na Kushoka Tools inayojihusisha kutengeneza mashine za kuzalishaji nishati mbadala, Leonard Kushoka alisema mafunzo hayo yanafadhiliwa na Taasisi ya Tulia Trust ambayo inamilikiwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Alisema vijana wanafundishwa kutumia takataka mbalimbali zinazozalishwa kutengeneza nishati hiyo ambayo ni mkaa safi ambao hauna harufu mbaya.

"Tumefika Mkoa wa Mbeya kwa ufadhiri wa Spika wa Bunge na Mbunge wa Mbeya mjini, Dk. Tulia Ackson kuwapatia elimu vijana zaidi wakishajifunza tutawafungia mashine ya kisasa yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa kilo 1,000 mpaka 3,000 kwa siku,"alisema Kushoka.

Alisema uwepo wa mradi utakuwa fursa kwa vijana kuisaidia Serikali kufikia malengo ya kupiga marufuku jamii kutumia nishati ya mkaa inayotokana na uchomaji wa miti ovyo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM ) Wilaya ya Mbeya Mjini, Clement Mwandembwa alisema mafunzo hayo yatawafanya vijana kujiajiri na hivyo kupunguza tatizo la ajira hasa katika Jiji la Mbeya ambako kuna vijana wengi.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo kwa kujitokeza kujifunza ili wapate eneo la kujiajiri na kuwa sehemu ya watu wanaolinda mazingira.

Ofisa Maliasili na Mazingira wa Jiji la Mbeya, Agape Mwantake alisema uwepo wa fursa hiyo utasaidia utunzaji wa mazingira kwa kutokata miti ovyo kwa ajili ya kuchoma mkaa katika maeneo ya hifadhi za misitu ya asili.





# Dk. Mwinyi: Serikali inahamasisha fursa za lugha ya Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inahamasisha na kushajihisha wananchi kuzitumia vyema fursa za lugha ya Kiswahili na kuzifanyia kazi ya kutafsiri kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Maimbo Mndolwa, aliyefika kujitambulisha na ujumbe wake baada ya kuchaguliwa kuongoza kanisa hilo Februari mwaka huu, kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Dk. Mwinyi alisema, lugha ya Kiswahili inafursa nyingi duniani kutokana na kazi za ukalimani, hivyo aliwataka Wazanzibari na Watanzania kutumia fursa hizo kwa wingi na kuahidi ushirikiano baina ya kanisa na Serikali katika kuwashajihisha vijana kuzichangamkia.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alimuahidi Askofu Mndolwa kuzungumza na wahusika wa Kamisheni ya Kiswahili ili kuona namna ya kuboresha ushirikiano baina ya serikali na kanisa hilo.

Alisema, Serikali ya Zanzibar ina uhusiano wa muda mrefu na kanisa hilo, hivyo aliutaka uongozi huo mpya kuendeleza ushirikiano wao na serikali hasa kwenye suala la kuendelea kuhubiri amani, umoja na mshikamano.

Akizungumzia masuala ya kuboresha utalii Zanzibar, Rais Dk. Mwinyi alilipongeza Kanisa Anglikana Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwavutia watalii wengi sambamba na kupongeza hatua ya kanisa hilo kuwaalika watu wakubwa duniani kuja Zanzibar hali itakayozidi kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kimataifa pamoja na kukuza sekta ya utalii.

Pia, Rais Dk. Mwinyi alilipongeza kanisa hilo kwa juhudi zake za kupinga harakati za biashara ya kuuza binadamu ambayo imeshamiri sana duniani sambamba na kumueleza Askofu Maimbo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaunga mkono hatua hiyo, wadau na wanaharakati wote wanaopinga udhalimu huo.

Naye, Askofu Mndolwa alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa maendeleo makubwa aliyoyafanikisha kipindi kifupi cha uongozi wake.

Askofu Maimbo alisema mpango wa kanisa hilo kutumia historia ya biashara ya utumwa Zanzibar, kama ni fursa adhimu ya kukuza utalii kwa Zanzibar kupitia kanisa hilo ambalo limekua kivutio kikubwa kwa watalii wengi wanaofika nchini.

Alisema Kanisa la Anglikana lina mpango wa kuwaalika mataifa makubwa akiwemo Gavana Mkuu wa Ujerumani kuja Zanzibar.

Alisema Ujerumani iliacha athari na historia kubwa ya biashara ya utumwa Zanzibar pamoja na mataifa mengine kwa lengo la kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa njia za utalii pia kuweka mkazo kwenye sekta hiyo.

Pamoja na kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuangalia uwezekano wa kuimarisha kiutalii maendeleo ya kanisa hilo kwa sababu ni kivutio kikubwa kwa wageni na kuiomba Serikali kuangalia namna ya kufunga mashine za kudhibiti mapato yanayotokana na utalii ili kuzuia mianya ya kodi za serikali zisipotee mikononi mwa wasiohusika.

Akizungumzia umuhimu wa lugha ya Kiswahili kimataifa, Askofu Maimbo alimuomba Dk. Mwinyi ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamisheni ya Kiswahili kushirikiana kuwaandaa vijana ili wakawe wakalimani wazuri kimataifa, kwamba nafasi nyingi zimechukuliwa na Wakenya na Wakongo.

Alisema Tanzania ina fasaha nzuri ya lugha ya Kiswahilli, hivyo aliziomba Serikali za SMZ na SMT kwa ushirikiano wa Kanisa Anglikana Tanzania kuitumia fursa hiyo kwa Watanzania kunufaika.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA), Hamza Johari (katikati), akifuatilia matukio katika kilele cha maadhimisho ya Tamasha la Kizimkazi, Paje Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi vyuo vikuu watakiwa kufuata sheria, taratibu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said, amewataka wanafunzi wa vyuo vikuu wanaokwenda kwenye mazoezi ya vitendo kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu zinazowekwa katika ofisi walizopangiwa.

Alisema hayo wakati wa kikao na wanafunzi kutoka vyuo vya elimu ya juu kwa ajili ya mazoezi ya vitendo yaliyofanyika katika Wizara ya Elimu Mazizini Zanzibar.

Aliwataka kuhakikisha wanafuata nidhamu zote za ofisi ikiwemo muda wa kuingia na kutoka kazini.

Aidha, aliwataka kufuata miongozo kwasababu ndiyo njia sahihi ya kufanikiwa katika mafunzo yao.

Pia, aliwataka kuhakikisha wanatunza siri za ofisi wanazoenda kuzifanyia kazi kwa sababu ndiyo njia sahihi ya mafanikio.

Wakizungunza na waandishi wa habari wanafunzi hao walisema ni jambo la kuigwa mfano kuona kiongozi wa wizara anakua karibu nao kwa kuhakikisha wanafuata njia sahihi kwa kipindi chote cha kazi zao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Asha Ali alisema watahakikisha wanafuata taratibu zinazowekwa ili kufikia malengo yao.

# JUWAUZA yakoshwa uteuzi wajumbe Tume ya Uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Bakar Hamad, amesema wanapongeza uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kwamba umezingatia wajumbe jumuishi.

Akizungumza na Nipashe Ofisini kwake Zanzibar, Bakar alisema wajumbe wa tume hiyo waliochaguliwa ni watu wenye uweledi na ujuzi na tayari wana uzoefu mkubwa wa kufanya kazi katika tume mbalimbali, hivyo utaalamu wao wanaamini watautumia vizuri katika Tume ya Uchaguzi.

"Imani yetu ni kwamba kilio cha wananchi juu ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi cha muda mrefu kitakwenda kupungua kutokana na uweledi wao wa kazi wanazozifanya" alisema Bakar.

Aidha, alisema wameangalia tume ilivyochaguliwa kuwa jumuishi ikiwa na wajumbe wanawake wawili, kwamba kipindi kilichopita kulikuwa na mjumbe mmoja tu mwanamke.

"Angalau kipindi hiki wanawake wawili mara hii tume iliyopita ilikuwa na mwanamke mmoja ingawaje watu wenye ulemavu hawajajumuishwa tungependa kuona katika tume kuna angalau uwakilishi wao wakati ambao tunazungumzia tume jumuishi" alisema Bakar.

Akitoa mifano ya umuhimu wa kuwa na tume yenye watu wenye ulemavu, alisema JUWAUZA ilishiriki kwenye uangalizi wa uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na wameshuhudia changamoto nyingi za watu wenye ulemavu kuanzia kwenye kampeni hadi siku ya upigaji kura.

"Kwenye kampeni watu wenye ulemavu wanapata shida sana kwa mfano wenye ulemavu wa ngozi wanashindwa kukaa, kusikiliza kampeni katika mikutano inayofanywa uwanjani wakati wa jua kali, hawana sehemu nyingine ya kusikiliza sera za vyama" alisema.

Aidha, alisema watu wenye matatizo ya kusikia hawana wakalimani, hivyo wanashindwa kusikia kinachozungumzwa, lakini wale wenye ulemavu wa viungo nao wanashindwa kwenda kwenye kampeni kutokana na kupakiwa kwenye gari na kushushwa sehemu mbali na uwanja na ikizingatiwa hawawezi kutembea umbali mrefu.

Akizungumzia suala la upigaji kura alisema ni changamoto kwa watu wenye ulemavu kutokana na kuwa baadhi yao wasioona wanapigiwa kura na watu ambao hawaaamini, hakuna mazingira wezeshi ya wao kuweza kupiga kura wenyewe.

Alisema watu hao lazima wasaidiwe lakini kuna wale wenye ulemavu wa viungo wanashindwa kuvifikia visanduku vya kupiga kura kwa sababu ni virefu na wengine ni wafupi.

Hata hivyo alisema imani yao changamoto hizo zinaweza kutatuliwa na tume kwa kuwa ina watu weledi.

HABARI KITAIFA



Meneja Masoko wa kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania na Rwanda, Sarah Munema (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu udhamini wa kampuni hiyo katika mbio za mbuzi 2023 zinazoandaliwa na Klabu ya Rotary na zinatarajiwa kufanyika Septemba 9 mwaka huu, ili kukusanya Sh. Milioni 320 za kufadhili wanafunzi wa elimu ya juu. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Bunge laridhia Azimio la biashara SADC

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

BUNGE limepitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini wa Afrika (SADC) ya mwaka 2012 huku wabunge wakitaka serikali kutoa elimu kwa wananchi ili kuondoa lawama kwa mambo yanayopitishwa na Bunge.

Wakichangia jana bungeni jijini hapa kuhusu azimio hilo, wabunge hao walitaka serikali ijikite katika utoaji elimu ili kuondokana na maneno, 'Tumeuzwa, tumekodishwa au kupangishwa".

Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, alisema serikali inatakiwa kuwekeza nguvu kubwa ya kuhakikisha watanzania wanaelewa nini nia thabiti ya serikali kwa kuwapa elimu.

"Usipomsaidia mtu vizuri kwenye akili akapata uongo na kuuweka kwenye akili yake kuja kutoa huo uongo alioweka moyoni ni tatizo, serikali kwenye maazimio kama haya yasiishie tu hapa lazima kuwe na program maalum ya kuelimisha Watanzania.

"Maazimio haya yamilikiwe na serikali kama mnavyotumilikisha wabunge, na watanzania wayamiliki ni mambo ya nchi yetu wayaelewe. Isiwe rahisi mtu anaambiwa tumeuzwa wengine presha zinapanda, mtu anaweza kutoka na hili azimio akasema mmekodishwa SADC au tumepangishwa, kumbe nia si hiyo, nia ni thabiti. Tutumie fedha kutoa elimu kwa watanzania," alishauri.

Mbunge wa Mkalama, Francis Mtinga, alisema: "Niiombe serikali ni kweli inapoleta suala Itifaki bungeni ni suala la kibunge, lakini serikali iwe na mtindo wa kuandaa wananchi kwamba sasa tunapelekea Itifaki fulani bungeni inayowahusu. Kwa sababu bungeni ni mahali pekee unaweza kumwita mwananchi au mdau na kumsikiliza.

"Serikali ijenge tabia ya kuhabarisha wananchi na wadau, sisi Bunge tunapowaita wanakuwa na uelewa na kutoa michango yao na linakuwa ni jambo letu wote tunapolipitisha. Wanapokuwa hawana habari alafu tunapitisha jambo, tukitangaza kwa taratibu zetu za watu waje, wengine magazeti hawasomi, mitandao hawapitii, tukitangaza hawawezi kuja."

alitolea mfano kamati yao kwenye jambo hilo, ililazimika kuahirisha mara mbili kwa sababu watu wengine hawana taarifa.

"Serikali katika itifaki mbalimbali mnazotaka kuzileta bungeni, jengeni tabia ya kuhabarisha wadau na wananchi ili waje kutoa michango yao, ili tukipitisha linakuwa ni jambo letu na si la kutukana Bunge na kulaani Bunge kwa jambo ambalo tumepitisha kwa nia njema kwa nia ya kuwasaidia wao.

"Lakini kwa sababu hawakuwa na habari wanaona kama vile wamesalitiwa. Niiombe serikali ijenge hii tabia ili tuende kwa pamoja walau wawe wanafaidi hizi Itifaki wawe wanaelewa zimepita kwa nini? Na kwa manufaa gani? Na hivyo kuzitumia," alishauri.

Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, alisema wanapozungumzia soko la SADC ni kubwa ambalo Tanzania kwa mwaka 2022, iliuza bidhaa na huduma zaidi ya Sh. trilioni 4.5.

"Kabla ya kuridhia ni lazima tupewe mambo fulani tupewe majawabu. Tujiulize kwa nini azimio hili tangu lisainiwa na wakuu wa nchi mwaka 2012 leo ni miaka 11 halijawahi kuridhiwa, sababu zilizosababishwa ni zipi? mazingira yaliyokuwapo kwa nini halikuletwa kabla?.

"Rais Mstaafu Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete ambaye alisaini hii Itifaki mwaka 2012 amekaa madarakani miaka minne, hakuwahi kuleta hili azimio ndani ya Bunge liridhiwe, leo kwa nini linaletwa hapa bungeni?

"Sababu za kuchelewa ni nini? Kama kuna sababu za kurekebishwa mbona hatujaambiwa? Hii Itifaki tunayoridhia inakwenda kutibu nini? Mbona maandalizi ya ndani ya kuridhia Itifaki hii hayapo?" alihoji Mpina.

Kuhusu kuadimika kwa Dola Mbunge huyo alisema, "Katika sekta ya fedha nchi za SADC zinategemea Dola ambazo zimeadimika na maelezo ya serikali uwekezaji umeongezeka ndani ya nchi, watalii wameongezeka mara dufu. Dola zimekwenda wapi? Kama uwekezaji umeongezeka mara dufu na watalii wameongezeka."

Mpina alisema serikali ni lazima itatue tatizo la kuadimika kwa Dola na kwamba anavyoona sababu ambayo haizungumziwi ni suala la ufisadi mkubwa ulioripotiwa na Financial Intelligence Unit (FIU) kuhusu miamala ya zaidi ya trilioni 280.

"Inawezekana dola zetu zimetoweshwa kupitia benki au mipakani leo hii nchi haina dola," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Hassan Aboud, alitaja serikali ianzishe kitengo maalum cha kuibua fursa zinazopatikana SADC na kuwasaidia wafanyabisahara kujua fursa katika nchi hizo wanachama na kuwawezesha kimitaji watoa huduma.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi alisema naye ana wasiwasi kwa nini itifaki hiyo imechelewa lakini kwa kuwa si jambo geni, mambo mengi Tanzania yamekuwa yakichelewa na kushauri ni vizuri kukiwa na fursa nzuri wajitahidi kwenda nazo kwa haraka.

Pia alishauri serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kuhakikisha inatumia fursa ya nchi wanachama wa SADC kusambaza dawa na iandae wataalam wambao watakwenda kufundisha Lugha ya Kiswahili.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alitaja manufaa ya Itifaki hiyo kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji kwa wakulima, ajira na thamani ya mauzo ya kilimo kupitia kuimarika kwa huduma wezeshi za malipo, usafirishaji na mawasiliano.

Pia kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani milioni 360 katika jumuiya ya SADC.

"Lengo la itifaki hiyo ni pamoja na; kurahisisha ufanyaji biashara ya bidhaa za sekta zote za viwanda, kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

Alisema katika kutekeleza suala hilo, Wakuu wa Nchi na serikali za SADC watia saini Itifaki ya Biashara ya Huduma Agosti 18, 2012, Maputo nchini Msumbiji.

"Baada ya utiaji saini huo nchi wanachama zilianza awamu ya kwanza ya majadiliano ya utegezaji wa masharti ya biashara ya huduma yakihusisha sekta sita za kipaumbele ambazo ni mawasiliano, fedha, utalii, uchukuzi, nishati na ujenzi na ya pili yaliyoanza mwezi Oktoba, 2022 na bado yanaendelea yakihusisha sekta sita za huduma za biashara, usambazaji, elimu, mazingira, afya ya jamii, burudani, utamaduni na michezo," alisema.

Alisema hadi Januari, 2022, nchi wanachama 11 kati ya 16 sawa na theluthi mbili, zilikuwa zimeridhia itifaki hivyo kuipa nguvu ya kisheria kuanza kutekelezwa.

"Nchi ambazo hazijaridhia itifaki hiyo ni anzania, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Madagascar na Comoro. Serikali kupitia Baraza la Mawaziri imeona ni muhimu kuridhia Itifaki hii na hivyo, kupitisha mapendekezo hayo Machi 3, 2023," alisema.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**COSMAS MORIS HONERA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya LANDROVER DEFENDER 110 yenye namba za usajili T 657 ALP chasis namba SALLDHAFMA962574 engine namba 16L19463A,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**PHQ/PWA/BAG/284/2023**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**JOYCE G MALUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1434/0033** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya PIUS mwaka 2014 Yeyote Atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/170581/2021**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**MRISHO RAMADHANI IDDY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 1786/0032 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondary ya LUICHE mwaka 2014. Yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa KGI/RB/541/023.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**SALOME EDWARD YUYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0563-0273 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule/kituo TTC TABORA ya mwaka 2004 Yeyote Atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa PHQ/DAR/KIN/6432/2023**

**PASSPORT IMEPOTEA**



**TUPOKIGWE USAJE MWAKAPALA** anatangaza kupotea kwa passport yake yenye No. TAE380648 iliyotelewa 15 January,2021 na kuisha muda wake 15 January 2031. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi:
**Taarifa ya Polisi MBE/KYE/RB/253033 /2023.**

# India yaomba Marekani kuachia fedha zake

**MUMBAI,** INDIA

NCHI ya India imeiomba Marekani iruhusu kuachiwa kwa fedha zake kiasi cha dola milioni 26, ambazo ni za kampuni mbili zinazoendesha biashara ya almasi.

Kulingana na taarifa za serikali ya India, ilieleza Marekani ilizizuia fedha hizo kutokana na kampuni hizo kudaiwa kufanya biashara na kampuni ya almasi ya Russia inayoitwa Alrosa ambayo imewekewa vikwazo.

Fedha hizo zilizuiliwa mwanzoni mwa mwaka huu kufuatia vikwazo vya Marekani dhidi ya kampuni hiyo vilivyowekwa Aprili mwaka 2022 na ofisi ya hazina ya Marekani inayodhibiti mali za kigeni.

Baadhi ya wanachama wa kundi la nchi tajiri la G7 walipitisha vikwazo dhidi ya biashara ya almasi kwa kampuni za Russia. **DW**

# Ulaya waijadili kuiwekea vikwazo Niger

**TOLEDO,** HISPANIA

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya wanakutana mjini Toledo nchini Hispania, kwa lengo la kujadili hali inayoendelea katika taifa la Niger.

Mkuu wa sera za mambo ya nje wa Umoja huo Joseph Borrell, atapendekeza juu ya vikwazo dhidi ya waliohusika na mapinduzi ya kijeshi.

Borrell alisema uamuzi wa kuweka vikwazo ambavyo vitakavyopitishwa na Umoja huo unalenga kwenda sambamba na hatua zozote zitakazochukuliwa na nchi za kikanda za jumuiya ya kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS).

Mkuu huyo wa sera za nje, akizungumza mbele ya waandishi habari baada ya mkutano wa mawaziri wa ulinzi juzi alisema watafuata njia ya kujaribu kutekeleza vikwazo kama ilivyoamuliwa na ECOWAS.

Pia alisema umoja huo unaweza kufikiria kutoa msaada wa fedha kwa HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/ecowas-yasema-la-kwa-pendekezo-la-utawala-wa-kijeshi-niger/a-66595327" ECOWAS iwapo itataka kuingia kijeshi nchini Niger na ikiwa itaomba msaada huo. **DW**

# Jenerali Nguema ateuliwa kuongoza kijeshi Gabon

**LIBREVILLE,** GABON

VIONGOZI wa kijeshi waliochukua madaraka baada ya kuipindua serikali nchini Gabon, wamemteua Jenerali Brice Oligui Nguema kuwa kiongozi wa mpito wa taifa hilo la Afrika Magharibi.

Baada ya mapinduzi hayo yaliyofanyika juzi, Jenerali Nguema alionekana akibebwa na wanajeshi wenzake kama mshindi katika mitaa mbalimbali ya mji mkuu wa Libreville.

Rais Ali Bongo ambaye amewekwa kizuizini, ameonekana kwenye video akiwa nyumbani kwake akitoa wito kwa marafiki zake duniani kote wapige kelele kwa niaba yake.

Mkazi mmoja wa Libreville alizungumza na BBC kuhusu mapinduzi hayo na kueleza mwanzoni aliogopa, lakini baadaye alihisi furaha.

"Niliogopa kwa sababu ya kutambua kwamba ninaishi kupitia mapinduzi, lakini furaha ni kwa sababu tumekuwa tukingoja kwa muda mrefu serikali hii kupinduliwa," alisema.

Aliongeza "Mazingira ya Libreville ni ya kipekee, kuna furaha nyingi hatimaye kukombolewa kutoka kwa familia ya Bongo pamoja na wasiwasi kidogo,"

Alisema, raia wa Gabon walikuwa wakisema walifurahi kumchagua mbwa badala ya Bongo, na kwa namna fulani wamefurahi.

"Tunafurahi kwa sababu jeshi letu lilifanya hivi wenyewe na inatufanya tuhisi kama tunaelekea kwenye suluhisho ambalo litamzingatia kila mtu." alisisitiza mkazi huyo.

Wakati huo huo, Ufaransa, Uingereza na Umoja wa Afrika zimelaani mapinduzi ya kijeshi yaliyotokea nchini Gabon na kuhimiza kuwepo kwa suluhu ya amani katika mzozo huo uliojitokeza baada ya uchaguzi mkuu kufanyika katika taifa hilo.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, mwenyekiti wa kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki, ameyataja mapinduzi hayo ya kijeshi kama ukiukaji wa wazi wa sheria na mkataba wa Afrika kuhusu uchaguzi, demokrasia na utawala.

Faki ametoa wito kwa jeshi kuhakikisha usalama wa Rais Ali Bongo, familia yake na baadhi ya maofisa waliokuwa wakimuhudumia.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres pia amelaani mapinduzi hayo.

Kupitia taarifa, Guterres ametoa wito kwa wahusika wote kushiriki katika mazungumzo jumuishi na kuhakikisha kuwa utawala wa kisheria na haki za binadamu zinaheshimiwa.

Jeshi lilitwaa madaraka nchini Gabon juzi baada ya viongozi wa kijeshi walipotangaza kwenye televisheni ya kitaifa kuwa taasisi zote za serikali na matokeo ya uchaguzi yamefutwa kutokana na udanganyifu na kwamba mipaka ya nchi hiyo imefungwa. **BBC**



Wafanyakazi wa kikosi cha uokoaji wakitafuta watu walioathirika ndani ya jengo la ghorofa katikati ya jiji la Johannesburg, nchini Afrika Kusini jana. **PICHA: REUTERS**

# Watu 73 wateketea kwa moto

**JOHANNESBURG,** AFRIKA KUSINI

WATU 73 wamefariki dunia baada ya moto kuzuka na kuteketeza jengo moja mjini Johannesburg nchini Afrika Kusini jana.

Mamlaka nchini humo ilisema watu wengine zaidi ya 40 wamejeruhiwa na kukimbizwa hospitali kwa ajili ya matibabu.

Maofisa walisema haijafahamika ni nini kilisababisha moto huo katika jengo hilo la ghorofa tano katikati mwa jiji.

Msemaji wa huduma za dharura, Robert Mulaudzi, aliambia BBC kwamba wazima moto wamefanikiwa kuwaokoa baadhi ya watu waliokuwa ndani.

Alisema moto huo uliteketeza jengo hilo, na kwamba msako wa kuwatafuta waathiriwa wengine unaendelea.

Tunapanda ghorofa hadi ghorofa tukitafuta watu au kuokoa miili," alisema Mulaudzi.

Video iliyotumwa katika mtandao wa X, ambayo zamani ilijulikana kama Twitter, na Mulaudzi ilionyesha magari ya zimamoto na ya kubebea wagonjwa nje ya jengo hilo na huku madirisha yakiwa yameteketea.

Picha kutoka eneo la tukio zilionyesha baadhi ya miili iliyofunikwa ikiwa imejipanga karibu na jengo lililoungua.

Ripoti zinaonyesha waliokuwa wakiishi ndani ya jengo hilo walikuwa wahamiaji kutoka mataifa mengine ya Afrika.

Taarifa za ndani zilisema kuwa eneo lilipo jengo hilo ni kitongoji cha ndani ya jiji la Johannesburg ambacho kina sifa ya kuwa na majengo yaliyotekwa nyara na wababe, kama inavyojulikana na wananchi wa nchi hiyo.

Majengo hayo yalichukuliwa kinyume cha sheria na wahamiaji wasio na vibali.

Baada ya tukio hilo la moto, raia wengi wa Afrika Kusini wamelaani mashambulizi ya mtandaoni ya chuki dhidi ya wageni ambayo baadhi wameyatoa kwa waathiriwa na majeruhi. **BBC**

# DODOMA JIJI YAINGIA KAMBINI YAIPANIA MTIBWA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Dodoma Jiji kimeingia kambini jana kujiweka sawa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar inayotarajiwa kuchezwa Septemba 15, Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Kikosi hicho ambacho kimetoka kupoteza mchezo wao uliopita wa ligi kuu dhidi ya Simba, kimepania kufanya vizuri mbele ya wakata miwa hao wa manungu, Morogoro.

Kocha Msaidizi wa Klabu hiyo, Kassim Liogope amesema wakiwa kambini kujiandaa na mchezo huo wanatarajia kucheza mechi mbili au tatu za kirafiki ili kuwarudisha wachezaji wao kwenye hali ya upambanaji kwani watakua wamekaa bila kucheza mchezo wowote w akimashindano kwa zaidi ya siku 24.

"Tayari tumeshaanza kambi na maandalizi kwa ajili ya mechi zijazo za ligi, tunajua mechi yetu ya mwisho dhidi ya Simba tulipoteza lakini hii inayofuata dhidi ya Mtibwa tunacheza nyumbani na sisi huwa hatupendi kupoteza tukiwa kwetu,


"Tuna siku kama 24 au 25 za kusubiri, hivyo hatuwezi kukaa hivihivi lazima tupate mechi za kirafiki mbili au tatu ili kuwarudisha wachezaji katika hali yao ya kawaida," alisema Liogope.

Dodoma Jiji imecheza mechi mbili za Ligi Kuu mpaka sasa ikashinda moja mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union na kupoteza mabao 2-0 dhidi ya Simba na inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi tatu, mabao mawili ya kufunga na kufungwa mabao matatu.

Wakati huo huo, dirisha la usajili kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Championship, First League na Ligi ya Wanawake limefungwa jana Agosti 31.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), hakuna muda wa ziada wa kuendelea na usajili.

Dirisha hilo lililofunguliwa Julai Mosi lilizitaka klabu zote kufanya usajili ndani ya muda.




Muogeleaji mahiri, Collins Saliboko (kulia), akipokea mfano wa hundi ya dola za Kimarekani 5,000 kutoka kwa Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya Sukari Kilombero (KSCL), Fimbo Butallah, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, iliyotolewa na KSCL kuchangia sehemu ya ada yake, wakati akijiandaa kushiriki kozi ya Usimamizi wa Michezo katika Chuo Kikuu cha Indianapolis, nchini Marekani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *CWT kuimarisha michezo kwa walimu*

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimejipanga kuimarisha sekta ya michezo kwa walimu nchi nzima ili kuwaandaa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Hayo yamebainishwa jana na Makamu wa Rais wa CWT, Suleiman Komba, wakati akiipokea timu ya walimu ya Tanzania iliyotoka Botswana ilikokuwa ikishiriki katika mashindano ya michezo ya umoja wa vyama vya walimu wa nchi za Kusini mwa Afrika (SATO).

Komba alisema idadi ya walimu kutoka mikoa 16 walioenda kuiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo ni ndogo, hivyo watahakikisha wanapata idadi kubwa ya wawakilishi hao kwa ajili ya mashindano yajayo.

" Lengo letu ni kuongeza wigo wa ushiriki,tutahakikisha mikoa yote inapata wawakilishi ili kuongeza idadi ya walimu walioenda Botswana mwaka huu ifikie kubwa katika mashindano yajayo,"alisema Komba.

Alisema kuna wakati ratiba za mashindano huwa ni ngumu na inaweza kufanyika michezo minne tofauti kwa wakati mmoja katika viwanja tofauti hali hiyo inawafanya wakati mwingine kushindwa kufanya vizuri kwa sababu ya uchache wa wawakilishi.

Kutokana na hilo alisema ndio maana wamejipanga kupanua wigo wa washiriki katika michuano ijayo ili kuwa na timu kubwa ya washiriki ambao wanaweza kujigawa katika michezo mbalimbali.

Kwa upande wake Mratibu wa Shughuli za Chama Kimataifa,Prosper Lubuva, ameishukuru CWT kwa kujipanga kuongeza idadi ya wachezaji na bajeti ili kuongeza ufanisi zaidi katika michuano ijayo.

Alisema wakifanya hivyo,itawasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali ya upungufu wa idadi ya wachezaji ili kuweza kugawa wachezaji katika kila mchezo ambao wanashiriki.

Alifafanua zaidi ya kuwa,katika michuano ijayo wamejipanga kuhakikisha wanaongeza idadi ya washiriki ili kuwa na timu moja katika kila mchezo ambao watapangwa kushiriki katika michuano hiyo ambayo hufanyika kila mwaka.

Kwa upande wake Mwalimu Kabula Kazimoto mmoja wa washiriki wa mashindano hayo kutoka jijini Mwanza alisema, ushiriki wa walimu ni muhimu katika mashindano hayo huku akisisitiza umuhimu wa kambi katika kuhakikisha walimu wanapata muda zaidi wa maandalizi.

Katika mashindano hayo,CWT ilishika nafasi ya Nne kati ya nchi 11 ambazo zimeshiriki mashindano hayo yaliyoanzishwa rasmi mwaka 1990 ambayo yalilenga kuwasaidia walimu kuimarisha afya, kushirikiana na kujadili kwa pamoja changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Alisema mashindano hayo kwa mara ya kwanza yalifanyika hapa nchini katika Jiji la Dar es Salaam Mwaka 2016.

## JKT Queens yaapa kuvunja rekodi ya Simba Queens Ligi ya Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutwaa Ubingwa wa Kombe la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Mkurugenzi wa Ufundi wa JKT Queens, Bakari Shime amesema watakwenda kufanya maandalizi kabambe ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika ili kuvuka rekodi iliyowekwa na Simba Queens msimu uliopita.

Akizungumza juzi nchini Uganda mara baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa CECAFA kwa kuibwaga CBE ya Ethiopia kwa mikwaju 5-3 ya penalti baada ya timu hizo kutoka suluhu katika mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa FUFA TC, Njeru nchini Uganda, Shime alisema baada ya kutwaa ubingwa huo wamepata tiketi si ya kuiwakilisha Tanzania tu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake, bali ukanda wote wa CECAFA, hivyo wanakwenda kufanya maandalizi kabambe ili wasiwaangushe watu wa ukanda huo.

"Niwapongeze Watanzania wote kwa ushindi huu, niwapongeze viongozi, benchi la ufundi na wachezaji, timu yetu ilikuwa inacheza mechi moja baada ya nyingine kulingana na ubora wa timu tuliyokuwa tunacheza nayo, katika mechi hii wameonyesha kiwango kikubwa sana hadi kufanikiwa kuwa mabingwa," alisema Shime na kuongeza,

"Kwa sasa tumepata nafasi ya kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa, tutarudi kukaa chini kuangalia pale ambapo tulitetereka tuparekebishe ili tukienda tuvuke pale ambapo timu ya Tanzania ilifika msimu uliopita," alisema Shime.

Naye kocha wa timu hiyo, Ester Chabruma alisema haikuwa kazi rahisi kutwaa ubingwa wa CECAFA mbele ya CBE ambayo ameitaja kuwa ni moja kati ya timu bora kwenye ukanda huu.

"Tumemaliza mechi yetu, tunashukuru kwa kuchukua ubingwa, mechi yetu ilikuwa nzuri na yenye ushindani, nilisema tangu awali CBE ya Ethiopia ni timu nzuri na kutakuwa na upinzani na kweli imekuwa hivyo, lakini sisi tulikuwa bora zaidi," alisema Chabruma.

Hii ni mara ya pili kwa timu ya Tanzania kutwaa ubingwa wa CECAFA ambapo msimu uliopita, Simba Queens ilitwaa ubingwa huo kwa kuifunga She Corporate ya Uganda bao 1-0 na kwenda kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa nchini Morocco ambako ilimaliza kwenye nafasi ya nne.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AL-ITTIHAD WAMKOMALIA SALAH
KLABU ya Al-Ittihad inaandaa dau la pauni milioni 118 kwa ajili ya Mohamed Salah, licha ya Liverpool kusisitiza kwamba mshambuliaji huyo raia wa Misri mwenye umri wa miaka 31 hauzwi. (***Mail***)

### KLOPP ATACHUKIZWA
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp atakasirika ikiwa timu hiyo itashawishiwa kukubali ofa ya Al-Ittihad ya Saudia kwa ajili ya Mohamed Salah wakati tarehe ya mwisho ya dirisha la uhamisho inapofungwa leo Ijumaa. (***Star***)

### SPURS WAMFIKIRIA EZE
KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Crystal Palace, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, baada ya uhamisho wa mshambuliaji wa Nottingham Forest, Brennan Johnson mwenye miaka 22, kukwama. (***Independant***)

### AMRABAT NA MAN UNITED
MANCHESTER United inataka kusajili kiungo kabla ya tarehe ya mwisho, huku mchezaji wa kimataifa wa Morocco wa Fiorentina, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27, akiwa lengo lao kuu. (***Mirror***)

### FIORENTINA IMEKATAA
KLABU ya Fiorentina imekataa ofa ya mkopo ya Manchester United ya pauni milioni 1.7 kwa Sofyan Amrabat lakini wanaweza kumuuza ikiwa watakuwa na lengo la kumnunua moja kwa moja. (***Mail***)

### HOJBJERG AWINDWA MAN
KLABU ya Manchester United pia imewasiliana na Tottenham Hotspur kuhusu kumnunua kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28. (***Sky Sports)***


### CHALOBAH AWINDWA
KLABU ya Bayern Munich imefanya mazungumzo na Chelsea katika jitihada za kumsajili beki, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24. (***Athletic***)

### TEDEN ATAKIWA LUTON
LUTON Town iko tayari kumsajili beki wa Manchester United, Teden Mengi mwenye umri wa miaka 21. (***Mail)***

### ODOI AKARIBIA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kufikia makubaliano ya kumchukua winga wa England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22 kutoka Chelsea. (***Guardian***)

### MCATEE ATAKIWA SHEFFIELD
KLABU ya Sheffield United inaongoza katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na England, James McAtee mwenye umri wa miaka 20 kwa kipindi cha pili cha mkopo katika klabu hiyo baada ya kukaa Bramall Lane msimu uliopita. (***Football Insider***)

### KONATE AWINDWA SAUDIA
KLABU ya Al-Ittihad imempigia simu beki wa Liverpool, Mfaransa, Ibrahim Konate mwenye umri wa miaka 24 kuhusu uwezekano wa kumsajili. (***RMC Sport)***



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI ULAYA




# FATI KUTUA BRIGHTON AKITOKEA BARCELONA

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati jana alitarajiwa kukamilisha uhamisho wa mkopo wa msimu mzima kwenda Brighton kutoka Barcelona.

**Fati amekuwa hana namba katika klabu ya Barcelona, ambayo inahitaji kutengeneza nafasi kwenye kikosi chao ili kumsajili beki wa pembeni wa Manchester City, Joao Cancelo kwa mkopo.**

Mkataba wa Brighton kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 haujumuishi kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

Tottenham pia walikuwa wakihusishwa na Fati, lakini inafahamika kuwa alifurahishwa na aina ya uchezaji wa Brighton chini ya kocha, Roberto de Zerbi.

Ikiwa mpango huo utakamilika kama ilivyopangwa, itakuwa mapinduzi makubwa kwa Brighton,

**Mshambuliaji huyo amekuwa hana namba kwenye kikosi cha mabingwa hao wa Hispania ambao watatumia kuondoka kwake ili kumsajili...**

ambao watakuwa wakicheza soka la Ulaya msimu huu kwa mara ya kwanza wakiwa wamefuzu kwanye Ligi ya Europa.

Fati, ambaye alizaliwa Guinea-Bissau lakini alichagua kuiwakilisha Hispania alikuwa sehemu ya kikosi chao cha Kombe la Dunia mwaka jana, anatazamwa na watu wengi kama mmoja wa wachezaji chipukizi wanaotegemewa zaidi kwenye mchezo huo.

Mwaka 2021, alisaini mkataba mpya na Barcelona hadi 2027 na ulijumuisha kifungu cha ununuzi cha euro bilioni moja.

Inaashiria mabadiliko makubwa kutoka kwa Fati, ambaye hapo awali alisita kuondoka katika klabu hiyo ya Katalunya msimu huu wa joto.

Barca, wakala wake, Jorge Mendes, na babake, Bori, wote wamekuwa wakishinikiza ahamie klabu nyingine kwa mwaka mmoja mahali pengine ili kupata nafasi ya kucheza.

Fati amekuwa akitokea benchi katika michezo mitatu ya kwanza ya Barca msimu huu lakini amekuwa na shida kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kocha Xavi Hernandez tangu apone majeraha ya muda mrefu kabla ya msimu wa 2022-23.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,148,6

MECHI KALI
ROMA
VERSUS
AC MILAN
1 | 2.73
X | 3.14
2 | 2.73

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Furahini Joasi - 0654 106 XXX
2. Ally Kidela - 0654 363 XXX
3. Jafari Homande - 0656 919 XXX
4. Shukuru Mwashilindi - 0677 413 XXX
5. Elifuraha Irunde - 0678 283 XXX
6. Marianus Lupembe - 0712 334 XXX
7. Shabani Mwapi - 0712 785 XXX
8. Avity Bakuza - 0713 324 XXX
9. Modesta Edmund - 0717 462 XXX
10. Medadi Kinyongo - 0719 228 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## NUNES KUTUA MAN CITY MANCHESTER, ENGLAND

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester City imefikia makubaliano ya mdomo na Wolves juu ya dili la pauni milioni 47.3 kumsajili kiungo Matheus Nunes.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 haujakubaliwa rasmi lakini ukikamilika, hakutakuwa na nyongeza.

Ofa ya awali ya City kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ilikataliwa wiki iliyopita, huku Wolves wakiaminika kutaka zaidi ya pauni milioni 60.

Nunes amekuwa hayupo mazoezini hivi karibuni baada ya kuweka wazi kuwa anataka kujiunga na kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola.

Aidha, Wolves wamekubali kumsajili kwa mkopo mchezaji wa kimataifa wa Man City na England chini ya miaka 21, Tommy Doyle, kukiwa na chaguo la usajili wa kudumu wa pauni milioni 4.3 ambao utajumuisha kipengele cha kuuza kwa City.

Mikataba hii miwili ni tofauti na inakuja baada ya City kukataa kufikia bei ya awali ya Wolves ya pauni milioni 60 pamoja na kumnunua Nunes.

City walitaka kuimarisha safu yao ya kiungo hata kabla ya Kevin de Bruyne kupata jeraha la misuli ya paja ambalo linaweza kumweka nje kwa miezi minne.

Lucas Paqueta wa West Ham alikuwa chaguo kabla ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 25 kuingia kwenye mzozo na Chama Cha Soka Cha England kwa ukiukwaji wa sheria za kamari.

Kocha wa Wolves, Gary O'Neil alisema baada ya ushindi wa Jumanne wa Kombe la Carabao dhidi ya Blackpool kwamba alitarajia Nunes kusalia katika klabu hiyo zaidi ya tarehe ya mwisho ya uhamisho leo Ijumaa.

Klabu hiyo ya Midlands ilimsajili Nunes kwa mkataba wa miaka mitano msimu uliopita wa majira ya joto, na kulipa pauni milioni 38 kwa Sporting Lisbon.

Alikuwa mtu muhimu katika kipindi cha pili cha msimu uliopita ambapo Wolves walifanikiwa kukwepa kushuka daraja, na kumaliza katika nafasi ya 13 kwenye msimamo.

# Balogun asaini mitano Monaco kutoka Arsenal

**LONDON,** England

MONACO wamekamilisha usajili wa pauni milioni 35 wa mshambuliaji Folarin Balogun kutoka Arsenal kwa mkataba wa miaka mitano.

Fowadi huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 22 anarejea Ufaransa baada ya kufunga mabao 22 kwa mkopo akiwa Reims msimu uliopita.

Balogun hakuwa ameichezea Arsenal katika Ligi Kuu England mwanzoni mwa msimu huu licha ya mshambuliaji chaguo la kwanza Gabriel Jesus kuwa majeruhi.

Alisaini mikataba ya kulipwa na Arsenal akiwa na umri wa miaka 17 na alicheza mechi mbili za ligi kuu wakati wake akiwa na klabu hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa kwenye tovuti ya Arsenal ilisema: "Tunamshukuru Folarin kwa mchango wake kwa klabu, kupitia akademi yetu kwenye kikosi cha kwanza, na tunamtakia afya njema na furaha katika sura yake mpya huko Monaco."

Mzaliwa huyo wa New York, Balogun alihamia London alipokuwa mtoto na alikua kupitia mfumo wa akademi ya Arsenal.

Alichezea timu za kundi la wachezaji chini ya umri wa miaka 21, akicheza mechi 13 katika kiwango hicho, kabla ya kuchagua kuchezea Merekani kwenye timu ya wakubwa.

Balogun alikuwa na muda wa mkopo kule Middlesbrough na Reims, na alihusishwa na Chelsea kabla ya Arsenal kukubali ofa ya Monaco.



43,241/-

# GAMONDI AMUONDOA SKUDU KWENYE MIPANGO YAKE

**Na Saada Akida**

KOCHA wa yanga, Miguel Gamondi amesema kwa sasa winga nyota wake Mahlatsi Makudubela 'Skudu' hayupo kwenye mipango yake na amempa programu maalum kwa ajili ya kumuweka sawa kabla hajaanza kumtumia kwenye kikosi chake huku akisema hakuna mchezaji aliye juu ya timu.

Skudu alijiunga na Yanga kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Mallumo Gallant ya Afrika Kusini ambapo tangu amejiunga na timu hiyo amefanikiwa kucheza mechi moja ya kimashindano kabla ya kuumia goti ambalo lilimpelekea arejee kwao Afrika Kusini kabla ya kurudi tena nchini wiki iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema ameamua kumpa program maalum ya mazoezi kwa ajili ya kurudisha utimamu wake kutokana na majeraha aliyopata kabla kumjumuisha kwenye mipango yake ya michezo iliyopo mbele yake.

"Skudu amerejea na ameshajiunga na timu lakini kwa sasa amekuwa akifanya mazoezi ya peke yake kwa sababu nimetaka afanye hivyo ili kuweza kurudisha utimamu kabla ya kumrudisha katika kundi la wachezaji wengine, najua ni mchezaji mzuri lakini siwezi kumrudisha moja kwa moja kwa kuwa ametoka kwenye majeruhi na hakuwa na timu," alisema gamondi na kuongeza,

"Naamini atarudisha kiwango chake na kuwa bora, ni mchezaji mzuri lakini kitu kikubwa ambacho tunaweza kuangalia kwa sasa ni wachezaji kuwa kwenye levo moja ya utimamu ili kuweza kwenda sawa na ratiba ya mashindano yaliopo mbele yetu, wiki moja ya mazoezi ya gym naamini itamrudisha kwenye hali yake kimwili," alisema Gamondi.

Gamondi alisema kwenye timu yake anataka nidhamu na kujituma muda wote na hakuna mchezaji mkubwa zaidi ya timu na muda wote amekuwa akiwaambia hivyo wachezaji wake mazoezini na hata kwenye kambi yao.



Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan akizindua mradi wa ujenzi wa uwanja wa michezo kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 utakaogharimu Shilingi Bilioni moja, katika eneo la Kibuteni, Kizimkazi, Kusini Unguja. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Camel Oil, Edha Abdallah ambao ndio wadhamini wakuu wa ujenzi huo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## *Robertinho awaandalia 'suprise' Power Dynamos*

INATOKA UK 24

nafasi zinazopatikana kwani amegundua wanatengeneza nyingi lakini wanashindwa kuzitumia.

"Tumecheza mechi mbili za ligi, ila mechi tulioshinda mabao 2-0 tulikosa mabao mengi tukiwa ndani ya boksi, Simba ni timu kubwa inatakiwa kucheza vizuri na kushinda mechi ikitumia nafasi zinazopatikana, hilo tunalifanyia kazi," alisema Robertinho.

Aidha, Robertinho alisema kikosi chake kinatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki na kama mambo yakienda vizuri huenda kesho Jumamosi ikateremka dimbani.

"Tunataka kulinda utimamu wa mwili na pumzi za wachezaji wetu baada ya 'pre season' ya nchini Uturuki, kwa maana hiyo nadhani tutakuwa na mechi kama mbili za kirafiki, Jumamosi ijayo, Jumatatu au Jumatano, na nafikiri tutapata timu nzuri za kutupima kwa sababu tuna michuano mingi, Ligi ya Mabingwa tukiingia hatua ya makundi na African Super League tutakuwa na mechi nyingi, kwa hiyo ni lazima tujiandae vizuri," alisema.

Katika hatua nyingine uongozi wa Simba upo kwenye mchakato wa kutafuta nchini jirani au sehemu sahihi ndani ya nchi kwa ajili ya kwenda kuweka kambi ya muda mfupi kabla ya kucheza mechi ya kwanza ya msimu wa 2023/24 ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia. Hatua hiyo ni kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa ili na kufikia malengo yao msimu huu ya angalau kucheza hatua ya nudu fainali. Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema Kenya ni moja ya nchi ambayo imekuwa ikitajwa na menejimenti ili kwenda nchini humo kuweka kambi ya muda mfupi.

Simba itacheza na Power Dynamos Agosti 16 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika kuwania nafasi ya kuingia hatua ya makundi.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/09/2023 | 19:30 | Brighton & Hove Albion vs Newcastle United | 2.50 | 3.55 | 2.50 |
| 02. 02/09/2023 | 19:45 | Go Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.60 | 3.60 | 2.39 |
| 03. 02/09/2023 | 20:00 | Portimonense SC vs Estrela Amadora | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 04. 03/09/2023 | 14:00 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.36 | 3.45 | 2.75 |
| 05. 03/09/2023 | 14:30 | KAA Gent vs Club Brugge | 2.32 | 3.55 | 2.70 |
| 06. 03/09/2023 | 15:00 | FC Andorra vs Tenerife CD | 2.19 | 3.00 | 3.45 |
| 07. 03/09/2023 | 16:00 | Kalmar FF vs Mjallby AIF | 2.25 | 3.00 | 2.90 |
| 08. 03/09/2023 | 17:00 | Union Saint-Gilloise vs Royal Antwerp FC | 2.31 | 3.35 | 2.85 |
| 09. 03/09/2023 | 17:15 | RCD Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.00 | 3.00 | 2.40 |
| 10. 03/09/2023 | 17:30 | GD Chaves vs Moreirense FC | 2.29 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 03/09/2023 | 17:30 | Estoril Praia vs Boavista Porto | 2.38 | 3.20 | 2.90 |
| 12. 03/09/2023 | 17:30 | FC Basel 1893 vs FC Zurich | 2.55 | 3.35 | 2.33 |
| 13. 03/09/2023 | 18:00 | Stroemsgodset IF vs Stabaek IF | 2.15 | 3.35 | 2.80 |
| 14. 03/09/2023 | 18:30 | IFK Norrkoping FK vs Djurgardens IF | 2.65 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 03/09/2023 | 18:30 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.10 | 3.25 | 2.24 |
| 16. 03/09/2023 | 19:30 | KRC Genk vs RSC Anderlecht | 1.95 | 3.65 | 3.40 |
| 17. 03/09/2023 | 20:15 | Royal Charleroi SC vs St. Truidense VV | 2.17 | 3.35 | 3.10 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 01/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5670 | Daejeon Citizen vs Suwon City | 1.92 | 3.58 | 3.23 |
| 13:30 | 1655 | Daegu vs Gangwon | 1.95 | 3.22 | 3.47 |
| 18:00 | 5165 | AL Faiha vs Al Raed Club | 2.04 | 3.50 | 3.39 |
| 18:15 | 1136 | Al Ahli Doha SC vs Al Gharafa SC | 3.08 | 3.74 | 1.93 |
| 19:30 | 2729 | Sassuolo vs Verona | 2.07 | 3.55 | 3.50 |
| 19:30 | 3374 | Fortuna Dusseldorf vs Karlsruher SC | 2.03 | 3.70 | 3.15 |
| 19:30 | 3699 | Eintracht Braunschweig vs St. Pauli | 3.44 | 3.64 | 1.94 |
| 20:00 | 1162 | Odense vs Vejle BK | 1.78 | 3.68 | 4.13 |
| 20:00 | 5441 | Vikingur Gota vs AB Argir | 1.09 | 7.88 | 15.15 |
| 20:30 | 1924 | Nancy vs Niort | 2.02 | 3.29 | 3.50 |
| 20:30 | 2045 | Villefranche Sur Saone vs US Marignane | 1.73 | 3.57 | 4.44 |
| 20:30 | 2281 | FC Rouen vs -Orleans | 2.42 | 3.20 | 2.79 |
| 20:30 | 2751 | Cholet vs Epinal | 1.96 | 3.35 | 3.61 |
| 20:30 | 3208 | Avranches vs Nimes | 2.24 | 3.21 | 3.05 |
| 20:30 | 3257 | Alcorcon vs Racing Ferrol | 2.22 | 2.97 | 3.31 |
| 20:30 | 3599 | Cadiz CF vs Villarreal | 3.29 | 3.45 | 2.19 |
| 20:30 | 4220 | UMF Selfoss vs Grotta | 2.25 | 3.79 | 2.49 |
| 20:30 | 5068 | Chateauroux vs Dijon | 2.41 | 3.15 | 2.84 |
| 21:00 | 1294 | Helmond Sport vs Cambuur | 3.23 | 3.54 | 1.99 |
| 21:00 | 1483 | Adanaspor vs Kocaelispor | 2.25 | 3.28 | 2.77 |
| 21:00 | 1515 | Den Bosch vs Jong PSV | 2.23 | 3.44 | 2.82 |
| 21:00 | 1874 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 1.91 | 3.66 | 3.41 |
| 21:00 | 1919 | VVV Venlo vs De Graafschap | 2.52 | 3.48 | 2.44 |
| 21:00 | 2361 | FC Oss vs Groningen | 4.40 | 3.84 | 1.65 |
| 21:00 | 2386 | Al Ittihad Jeddah vs Al Hilal Riyadh | 2.77 | 3.50 | 2.36 |
| 21:00 | 2664 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.93 | 3.23 | 2.18 |
| 21:00 | 3286 | AL Riyadh vs AL Akhdood | 2.21 | 3.47 | 3.05 |
| 21:00 | 3513 | Maastricht vs Jong Ajax | 2.12 | 3.80 | 2.77 |
| 21:00 | 3527 | Telstar vs FC Eindhoven | 2.18 | 3.36 | 2.95 |
| 21:00 | 5480 | Jong Utrecht vs Roda Kerkrade | 3.17 | 3.58 | 2.00 |
| 21:00 | 5595 | Caykur Rizespor vs Fatih Karagumruk | 2.20 | 3.45 | 2.93 |
| 21:00 | 5748 | Kasimpasa vs Trabzonspor | 2.94 | 3.46 | 2.19 |
| 21:00 | 5921 | Emmen vs Dordrecht | 1.39 | 4.70 | 6.13 |
| 21:15 | 1709 | FC Aarau vs Stade Nyonnais | 1.57 | 3.95 | 4.56 |
| 21:15 | 5376 | FC Sion vs FC Baden | 1.22 | 5.64 | 8.87 |
| 21:45 | 1531 | OH Leuven vs Kortrijk | 1.69 | 4.07 | 4.07 |
| 21:45 | 1649 | Wexford Youths vs Finn Harps | 1.74 | 3.59 | 3.89 |
| 21:45 | 2296 | Caernarfon Town vs Gap Connahs Quay | 3.68 | 3.48 | 1.82 |
| 21:45 | 3417 | Cork City vs Sligo Rovers | 2.78 | 3.24 | 2.27 |
| 21:45 | 3660 | Shelbourne vs St Patricks | 2.57 | 3.02 | 2.57 |
| 21:45 | 3928 | Cobh Ramblers vs Treaty United | 1.74 | 3.63 | 3.83 |
| 21:45 | 4107 | Roma vs AC Milan | 2.73 | 3.14 | 2.73 |
| 21:45 | 4129 | Shamrock Rovers vs Bohemians FC | 1.70 | 3.58 | 4.14 |
| 21:45 | 4608 | Drogheda Utd vs UCD Dublin | 1.21 | 5.46 | 9.71 |
| 21:45 | 5666 | Waterford Utd vs Athlone Town | 1.39 | 4.54 | 5.85 |
| 22:00 | 1793 | Nantes vs Marseille | 4.42 | 3.74 | 1.80 |
| 22:00 | 5192 | Luton Town vs West Ham | 4.43 | 3.76 | 1.79 |
| 22:15 | 5270 | FC Vizela vs Gil Vicente | 2.17 | 3.39 | 3.04 |
| 22:30 | 3032 | Albacete Balompie vs Valladolid | 2.09 | 3.27 | 3.27 |
| 23:00 | 4718 | Almeria vs Celta Vigo | 2.67 | 3.39 | 2.62 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 1, 2023

Nipashe


UK. 21



## Fati kutua Brightonakitokea Barca



Mshambuliaji wa Singida Big Stars, Morice Chuku akiwania mpira na beki wa Kitayosce (chini) huku Marouf Tchakei akiangalia kwa karibu wakati timu hizo zilipoumana jana kwenye mchezo wa ligi Kuu Tanzania Bara kwenye uwanja wa Liti Mkoani Singida. Timu hizo hazikufungana. **PICHA: MTANDAO**

## Robertinho awaandalia 'suprise' Power Dynamos

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema tayari ameandaa mfumo atakaotumia katika mechi ya mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos utakaopigwa Septemba 16, Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola nchini Zambia na atawashangaza wapinzani wake hao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kocha huyo amesema watakwenda na mfumo wao ambao anaamini utampa matokeo mazuri lakini watakuwa na nidhamu kubwa kwenye mchezo huo na watakachowapa Power Dynamos ni 'Suprise'.

"Katika mechi yetu ya ugenini tutakwenda kucheza tofauti na tutakavyocheza nyumbani, huko tutakuwa na nidhamu kubwa ya ukabaji, kutakuwa na msitari mmoja wa mabeki, mwingine ni wa viungo wakabaji na viungo washambuliaji wote itabidi wacheze pamoja, tutacheza kwa kukaribiana na kuufinya uwanja na kama kwenye kushambulia tutakwenda kwa pamoja na kurejea haraka, baada ya hapo katika mechi ya marudiano tutaangalia nini tutafanya, lakini nyumbani tutataka kucheza kwa uhuru kila mchezaji akionyesha kipaji chake kwa sababu soka si vita ila ni sanaa," alisema Robertinho.

Aidha, kocha huyo alisema anaandaa mkakati wa kuhakikisha wachezaji wake wanatumia

INAENDELEA UK 23

# Yanga yafichua siri ya kugawa '5G'

## ●●● Mashabiki waambiwa kinachotokea sasa ni rasharasha tu, ubora wa benchi ni....

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imefichua siri ya kupata ushindi wa mabao matano '5G' kwenye michezo yake mitatu iliyopita kuwa ni ubora na mbinu nyingi za benchi lao la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Miguel gamondi.

**Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa klabu hiyo, Walter Harrison alisema sababu ny ingine ni usajili bora walioufan ya kulingana na mahitaji ya timu yao.**

Alisema mashabiki na wananchama wa klabu hiyo wanachokiona sasa ni rasharasha kwani kikosi hicho hakijafika kwenye kiwango ambacho benchi la ufundi linahitaji.

Walter alisema mabadiliko ya benchi la ufundi pamoja na kuingiza damu mpya kwenye kikosi hicho imekuwa chachu ya mafanikio kwenye timu hiyo ndani ya muda mfupi.

"Kiuhalisia hii ni Yanga tofauti na ya msimu uliopita, ukiangalia kuna mabadiliko ya benchi la ufundi na ya wachezaji kwa hiyo haiwezi ikafanana na ile, hiki ambacho kimekuwa kikitokea ni ubora ambao tumeweza kuwa nao kwa makocha wetu, kuanzia kocha mkuu na wasaidizi wake na kila idara ya ufundi, pamoja na viwango vya wachezaji ambao wamesajiliwa na klabu yetu, chini ya Rais wetu, Injinia Hersi Said," alisema Harrison na kuongeza.

"Kinachoonekana ni kwamba viongozi wetu wametuliza akili na kufanya usajili wa watu sahihi wenye ubora wa juu wanaohitajika kwenye timu na mwisho wa siku ndicho kinachotokea sasa hivi ambacho watu wanakishuhudia, tutaendelea kufanjya vizuri, yanga hii imeimarika zaidi" alisema Meneja huyo.

Alisema pamoja na ushindi mnono wanaoupata bado benchi la ufundi linasema timu hiyo haijakaa vizuri na kufikia ubora ambao wanauhitaji.

"Haya mnayoyaona sasa hivi bado, hii timu haijakaa vizuri, haijafika kwenye ubora tunaouhitaji na hii ni rasharasha tu mvua itanyesha baadaye," alitamba.

Aidha, aliwataka wanachama na mashabiki kuendelea kuipa sapoti timu ili iweze kufanya vyema na kuhifadhi vikombe vyake ilivyochukua msimu uliopita.

"Mashabiki waendelee kutusapoti kwani tunaahidi kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, siwezi kusema tutakuwa tunashinda mabao matano kila mechi, lakini tumejipanga kuwaandaa wachezaji kwa ajili ya kuwapa ushindi na burudani pia," alisema meneja huyo wa Yanga.

Yanga ilishinda mabao matano katika mechi tatu mfululizo, ikiichapa ASAS Ali Sabieh Djibouti mabao 5-1 katika mechi ya mkondo wa pili ya hatua ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika, ikashinda mabao 5-0 katika mechi mbili za ligi kuu ilizocheza dhidi ya KMC na JKT Tanzania.

Ushindi katika mechi hizo mbili umeifanya yanga kukaa kileleni kwenye msimamo wa ligi kuu ikiwa na pointi sita lakini uwiano mkubwa wa mabao ya kufunga.

Yanga sasa inajiandaa kucheza mchezo wake wa kwanza hatua ya kwanza ya ligi ya mabingwa Afrika dhidi ya Al Merreikh ya Sudan mchezo ambao wataanzia ugenini Septemba 16 kabla ya kurudiana jijini Dar es Salaa wiki moja baadae.

Kama itafanikiwa kuitupa nje timu hiyo katika matokeo ya jumla, itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwenye ngazi ya vilabu Afrika.



9 770856 541002 >